**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Tisa – Tarehe 10 Novemba, 2006**

*(Mkutano ulianza saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ILIYOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Mwaka ya Bodi ya Utalii Tanzania kwa Mwaka 2004/2005 *(The Annual Report of the Tanzania Tourist Board for the Year 2004/2005).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 109

**Kukamilisha Ujenzi wa Madaraja na Barabara**

**MHE. YONO S. KEVELA** aliuliza:-

Kwa kuwa Madaraja ya Ilembula – Matowo na Daraja la Korintho - Ilembula yaliahidiwa kujengwa na kukarabatiwa mapema na Serikali pamoja na kukarabati barabara zinazounganisha vijiji hivi ambavyo ni kero kubwa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha madaraja hayo na barabara hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa ujenzi wa madaraja kwenye barabara za Ilembula- Korintho na Ilembula – Matowo pamoja na kukarabati barabara hizi ni mojawapo ya hatua kubwa ya kuwapunguzia kero wananchi wa Jimbo la Njombe Magharibi na Wilaya ya Njombe kwa ujumla.

Ujenzi wa daraja kwenye Mto Halali unaokatiza kwenye barabara ya Ilembula hadi Korintho ulikamilika rasmi mnamo mwezi wa Oktoba 2005 na uligharimu jumla ya shilingi 35.5 milioni na ujenzi wa daraja kwenye mto huo huo wa Halali unapokatiza kwenye barabara ya Ilembula hadi Matowo unaendelea na unategemewa kukamilika ifikapo mwezi Desemba 2006 kwa gharama ya shilingi 20.64 milioni. Aidha, barabara ya Palangawamu hadi Ilembula (km.12), ambayo inaunganisha Vijiji vya Palangawamu, Matowo na Ilembula ilifanyiwa matengenezo mnamo mwaka 2004 na hali yake siyo mbaya isipokuwa ujenzi wa daraja la Halali ambao unaendelea kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikishirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe inaendelea na ukarabati wa barabara ya Ilembula hadi Luduga yenye (km.9) kwa gharama ya shilingi 26.3 milioni na ukarabati unategemewa kukamilika mwishoni mwa mwezi Novemba 2006.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Daraja la Matowo – Ilembula limekuwa ni tatizo la muda mrefu na iliwahi kupewa mkandarasi na akafuja hela na sasa kuna mkandarasi mwingine amewekwa pale.

(a) Je, ni lini daraja hili litajengwa na hatua gani zilichukuliwa dhidi ya mfujaji wa hela za wananchi?

(b) Kwa kuwa Naibu Waziri, anasema barabara ya Igwachanya kwenda Palangawamu kupitia Luduga Mpaka Matowo ni nzuri wakati ukweli siyo hivyo, barabara ile ni mbaya haipitiki na haijawahi kulimwa. Je, Naibu Waziri, atanihakikishieje kwamba hizo barabara zitakamilika na hilo Daraja la Matowo litajengwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Daraja la Matowo – Ilembula sasa hivi linatengenezwa na kazi inaendelea. Kuhusu yule mkandarasi wa kwanza ikichunguzwa ikionekana ni kweli alifuja hela za wananchi hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Lakini mpaka sasa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa. Kuhusu barabara ya Matowo, ilitengenezwa mwaka 2004 kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi na iko katika hali nzuri kidogo siyo sana. Lakini, tukumbuke kwamba kila mwaka kuna *period maintenance* za barabara. Kwa hiyo, Halmashauri itakuwa inaendelea na ukarabati wa mara kwa mara ili barabara hii iweze kupitika kwa mwaka mzima. *(Makofi)*

Na. 110

**Kutengeneza Barabara Zilizoharibiwa na Magari Makubwa**

**MHE. RICHARD M. NDASSA (k.n.y. MHE. JACOB D. SHIBILITI)** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara zinazotengenezwa na kusimamiwa na Halmashauri zilizo nyingi zinahimili uwezo wa magari ya tani 10 tu na si zaidi:-

(a) Je, ni nani anayewajibika kutengeneza barabara na madaraja yaliyoharibiwa na magari ya zaidi ya tani 40 yaliyopitisha mizigo kwenda kwenye Mradi wa Maji wa Kahama na Shinyanga katika sehemu ya Buhingo, Seeke, Nyamayinza, Mbalamba, Ilalambogo, Isenengeja hadi Mwawile?

(b) Je, zitahitajika shilingi ngapi kuzirudisha barabara hizo kama zilivyokuwa?

(c ) Je, ujenzi wa barabara ya Misungwi – Kolomije inajengwa na nani, awamu ya kwanza iliyoishia Ibongoya B na iligharimu shilingi ngapi na sehemu iliyobaki ya Ibongoya A – Kolomije itajengwa kwa shilingi ngapi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mbunge wa Misungwi lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, ndiyo yenye mamlaka ya kutengeneza barabara na madaraja yaliyoharibiwa na magari makubwa yaliyokuwa yanapita barabara za Buhingo – Isesa na Mbarika – Mwalile ambazo zinapitia katika Vijiji vya Seeka, Nyamayinza, Mbalama, Ilalambogo, Isenengeja na Mwalile. Serikali kupitia Halmashauri husika imeshawasiliana na wakandarasi katika Mradi wa Maji wa Kahama/Shinyanga kutengeneza barabara hizi ambazo zimeharibiwa na magari yao na kampuni hiyo, wameahidi kuzitengeneza mara tu baada ya mradi kukamilika.

(b) Mheshimiwa Spika, gharama za matengenezo ya barabara hiyo iliyoharibika ni kama ifuatavyo:-

- Misasi – Mwasagela km 1.8 – itagharimu Sh. 14.4 milioni;
- Buhingo – Nyamayinza km 26.8 itagharimu Sh. 375.0 milioni;
- Mbarika – Ilujamate km 8.3 itagharimu shs. 77.4 milioni;
- Ilujamate – Mwawile (km 30.7 itagharimu shs. 274.5 milioni; na

Jumla ya gharama zote ni – Shilingi 741.3 milioni.

(c) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Misungwi – Kilomije inajengwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza kutoka Misungwi hadi Ibongoyo imejengwa na Wakandarasi wawili kwa gharama ya shilingi 180.5. Kutoka Misungwi hadi Mwambola *section* 1 imegharimu shilingi milioni 81,887,170.4 na imejengwa na *M/S Kashere Enterprices*. Kutoka Mwambola hadi Ibongoyo B (*section* 2) inagharimu shilingi 98.6 na kujengwa na M/S *MP Investment*.

Barabara ya Ibongoya A hadi Kolomije yenye urefu wa kilomita 7 itajengwa katika awamu ya pili kutoka na fedha za mradi wa *NRTP* na inakadiriwa kugharimu jumla shilingi 98,000,000/= tayari zabuni imetangazwa na kazi hiyo itaanza mara hiyo zabuni itakapokamilika.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa haya magari makubwa yamekuwa yakikwepa barabara kuu na kupitia njia za mkato kwa mfano barabara kutoka Shinyanga magari hupitia Hungumalwa kwenda Ngudu kwenda Magu na kukwepa ile barabara kuu ya kutoka Hungumalwa kwenda Mwanza. Kwa nini sasa Serikali ili madaraja yetu haya madogo madogo yasivunjwa na magari ya tani 10 Serikali itaonaje kama itaweka utaratibu wa kuweka mzani Hungumalwa badala ya kuweka mzani Isagala na Nyanguge ili magari haya yakija yapite kwenye mzani kabla ya kufika kwenye barabara hizi ndogo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, upande mmoja nakuhurumia kama mtu wa Ulanga kuyatamka haya Majina ya Kisukuma ya Vijiji vya huko lakini ndiyo kazi yenyewe. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, tuna upokea ushauri wake kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu tutaangalia kama kuna uwezekano wa kuweka mizani katika hiyo. (*Makofi*)

Na. 111

**Nyumba za Polisi Kambi ya Finya**

**MHE. MWADINI A. JECHA** aliuliza:-

Kwa kuwa ni muda mrefu sasa ujenzi wa nyumba za makazi ya Polisi Kambi ya Finya, umesimama na kwa kuwa nyumba za makazi ya polisi zilizopo *police line Wete* ni mbovu sana, zimechakaa na zinavuja mno wakati wa mvua hali ambayo inasababisha usumbufu mkubwa na kuhatarisha usalama kwa familia zinazoishi humo na kwa kuwa polisi wengi na hasa wa vyeo vya chini wana ari ya kujenga nyumba binafsi za kuishi lakini kipato chao ni kidogo:-

(a) Je, Serikali itamalizia lini ujenzi wa nyumba za polisi Kambi ya Finya?

(b) Je, ni lini Serikali itazifanyia matengenezo nyumba za *Police Line* ili ziwe na hali nzuri?

(c) Je, Serikali haiwezi kuwasiliana na taasisi za fedha nchini ili polisi wapatiwe mikopo ya kujenga nyumba zao za binafsi?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Mwadini Jecha, Mbunge wa Wete swali lake lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Jecha kuwa ujenzi wa nyumba za Finya, umechukua muda mrefu kukamilika kama ilivyo katika maeneo mengine nchini. Hii inatokana na uwezo mdogo wa Serikali kifedha. Lakini nia ya Serikali ni kuendeleza ujenzi wa nyumba za askari kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka huu zimetengwa jumla ya shilingi milioni 50 ili kuendeleza ujenzi wa nyumba za Kambi ya Finya. Nyumba hizo zitaendelea kukamilishwa kwa awamu kadri hali ya fedha katika bajeti ya Serikali itakavyoruhusu.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi, ina mpango wa kuzifanyia matengenezo na kujenga nyumba za polisi katika maeneo mbalimbali nchini zikiwemo nyumba za askari huko Wete. Mpango huo unatekelezwa kwa awamu kadri hali ya fedha inavyoruhusu. Serikali kila mwaka itaendelea kutenga fedha katika bajeti yake kwa ajili ya kazi hiyo.

Aidha, Jeshi la Polisi linaendeleza mazungumzo na taasisi za fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za askari na kipaumbele kitatolewa kwenye maeneo yenye mazingira magumu ya makazi ya askari.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kipato cha askari wetu ni kidogo kuwawezesha kujenga nyumba za kuishi. Kwa kutambua hilo Wizara ya Usalama wa Raia, imeanzisha *SACCOS* kwa kushirikiana na *CRDB*. Lengo la mfuko huo ni kuwawezesha askari kuchangia na baadaye kupata mikopo yenye riba nafuu kwa madhumuni ya kujiimarisha kiuchumi ikiwa ni pamoja na kujenga nyumba za kuishi. Aidha, Wizara ina mikataba na taasisi mbalimbali za fedha nchini zikiwemo Benki ya posta, *CRDB*, *NMB* na Benki ya Azania, ambazo zinatoa mikopo kwa wafanyakazi kwa udhamini wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, juhudi hizo zote za Serikali ni katika kuhakikisha kwamba kila askari mwenye nia ya kujiendeleza aweze kufanya hivyo.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la nyumba za Askari za Finya na *Polisi Line* Wete linafanana na tatizo la nyumba za Askari

za *Line Madungu* Chache Chake Pembe na zile za Mkoani. Je, Serikali inalijua hilo na kama inalijua ni lini itawasaidia askari hao pia?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimhakikishie kwamba Serikali inalijua hilo na katika jibu langu la msingi nilielezea kwamba nia ya Serikali ni kujenga nyumba za kuishi kwa nchi nzima kwa kadri hali ya uwezo wa kifedha itakavyowezekana. Kwa hiyo, nyumba za Madungu za Polisi linajulikana tatizo lake na nyumba za Mkoani tatizo lake linajulikana na nchi nzima tatizo lake linajulikana na ndiyo maana tunajipanga kuhakikisha tunaondoa tatizo hilo. (*Makofi*)

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ni kweli inaonyesha kwamba wana mpango madhubuti wa kuhakikisha kwamba wanajenga nyumba za askari Tanzania nzima. Lakini nina uhakika kabisa kwamba Serikali haitakuwa na uwezo wa kufika mpaka kwa wale askari wa vijijini mfano wa askari wanaoishi Kihurio, Ndungu, Gonja Maore na kadhalika. Je, wanawapa unafuu gani kwa sababu sasa wao sasa wanaishi kwenye nyumba za kupanga na inabidi wapewe japo kiasi cha zaidi waweze kulipia nyumba zile? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba nia ya Serikali ni kujenga nyumba za askari katika maeneo mbalimbali nchini. Lakini kutokana na uwezo mdogo wa kifedha ndiyo sababu kubwa inayokwamisha sababu kubwa inayokwamisha jitihada hizo. Tunalielewa vyema tatizo la askari huko vijijini na nia yetu hatua hatua ni kumaliza tatizo hilo ndiyo maana jeshi la Polisi limechukua hatua kuzungumza na vyombo vya fedha kwa nia ya kujenga nyumba za askari na hivi sasa mazungumzo yamefikia hatua za mwisho mambo yote yako Wizara ya Fedha, kwa nia ya kupata udhamini ili tuendeleze kujenga nyumba hizo. Kama nilivyosema tunaanzisha mfuko huu wa *SACCOS* kwa nia ya kuwasaidia askari wa chini na kuwasiliana na vyombo vingine vya fedha kwa nia hiyo hiyo ya kuwasaidia askari wa chini. Tutafanya kila jitihada tunajua matatizo hayo Serikali itachukua hatua kutatua tatizo la askari wa chini ili waweze kupata nyumba za kuishi katika makambi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Tunaendelea na matatizo ya makazi ya polisi.

Na. 112

**Uhaba wa Nyumba za Polisi**

**MHE. ALI KHAMIS SEIF** aliuliza:-

Kwa kuwa askari wengi hususan Polisi wanakabiliwa na tatizo la makazi na hivyo kulazimika kuishi mitaani wanakoishi raia na kwa kuwa Serikali ilijenga nyumba za kuishi Polisi eneo la Mfikiwa- Wawi, Wilaya ya Chake Chake ambazo hazikukidhi haja:-

Je, Serikali ina mpango wowote wa kujenga nyumba za polisi katika Wilaya za Mkoani Wete?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kabla hujajibu napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, kwamba kwa kuwa swali hili linafanana na nimekwisha mwona anaulizia nyongeza basi atapata nafasi mara baada ya mwuliza swali la msingi atakapomaliza nyongeza yake.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Ali Khamis Seif, kwamba pamoja na Serikali kujenga nyumba za kuishi za polisi eneo la Mfikiwa – Wawi, Wilaya ya Chake Chake, nyumba hizo hazikuweza kukidhi mahitaji halisi ya makazi kwa askari wetu huko Pemba. Tatizo hili ni la nchi nzima.

Nia ya Serikali ni kujenga nyumba za polisi katika kila Wilaya nchini ikiwemo Wilaya ya Mkoani na Wete. Lakini kutokana na uwezo mdogo wa Serikali, mpango huo utafanywa kwa awamu kadri hali ya fedha itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa askari kuishi makambini, Wizara inaendelea kufanya mazungumzo na Mashirika ya fedha hapa nchini kuona uwezekano wa kuingia mikataba na mashirika hayo ili kujenga nyumba za gharama nafuu kwa ajili ya askari wetu.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkoa wa Kusini Pemba umejengwa na Wilaya ya Chake na Mkoani na kwa vile Wilaya ya Chake tayari nyumba zimeshajengwa katika Kijiji cha Mfikiwa:-

(a) Je, Mheshimiwa Waziri anakubaliana nami kuwa nyumba zote zitakazoelekezwa katika kujengwa Mkoa wa Kusini Pemba zitaelekezwa Mkoani?

(b) Kwa kuwa hali za nyumba za Polisi Mkoani ziko katika hali mbaya sana je, Mheshimiwa Naibu Waziri atazifanyia lini matengenezo nyumba hizi?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali katika jibu la hivi punde katika swali lililopita kwamba nia ya Serikali ni kujenga nyumba za polisi katika kila Wilaya. Tunaangalia pale ambapo hali inakuwa ngumu zaidi. Tumeanza Pemba katika Wilaya ya Chake nia ni kuendelea katika Wilaya zingine kadri ya uwezo utakavyoruhusu. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge, avute subiri na huko Mkoani tutafanya jitihada tujenge hizo nyumba kutokana na hali halisi ya uwezo utakavyoruhusu.

Nakubaliana naye kwamba nyumba za Mkoani hali yake ni mbaya nimezipitia nimeziona kama ilivyo katika maeneo mengine hapa nchini. Kwa hiyo, jitihada ni hizo hizo nilizozieleza kwamba hatua mbalimbali zinachukuliwa za kukarabati nyumba hizi na kujenga nyumba nyingine kwa kadri hali halisi ya uwezo utakavyoruhusu.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na mategemeo ya Serikali ya kujiandaa kufanya matengenezo kwa nyumba zote nchi nzima. Lakini pia nina swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri, ningeomba anieleze katika mipango hiyo, ni umuhimu gani utatolewa kwa zile nyumba ambazo ziko hali mbaya zaidi kama za Ziwani Polisi ambazo zimechakaa sana na ziko katika hali mbaya sana. Atalifikiria vipi suala hilo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruksa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mohammed Rajab, Mbunge wa Jang'ombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, serikali imeliona tatizo la nyumba za Ziwani na hivi sasa mpango mahususi umeanzishwa kutatua tatizo hilo. Katika mazungumzo ya Jeshi la Polisi na taasisi ya fedha ya *NSSF*, hatua ya mwanzo ya ujenzi ni kujenga nyumba 60. Nyumba 50 pale Kurasini na 10 Ziwani Zanzibar. (*Makofi*)

**MHE. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Nyumba za Polisi za Finya mpaka leo hazijapata umeme ziko gizani je, litafikiriwa lini suala hilo la nyumba za Finya? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nyumba za Finya zina tatizo la umeme. Lakini tayari tathmini ya mahitaji ni shilingi milioni 21 Wizara inafanya utaratibu wa kutatua tatizo hilo ili Kambi ya Finya ipate umeme.

Na. 113

**Zana za Kilimo kwa Wakulima**

**MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO (k.n.y MHE. MOHAMED S. SINANI)** aliuliza:-

Kwa kuwa wakulima wa Mikoa ya Kusini wapo nyuma kiuchumi kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwa mstari wa mbele katika vita ya kuwakomboa ndugu zetu wa Msumbiji; na kwa kuwa wakulima wengi wanashindwa kumiliki zana za kisasa za kilimo kama matrekta:-

Je, Serikali itawasaidiaje wananchi hao kuinua hali zao kimaisha kwa kuwapatia zana bora za kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHIRSTOPHER K. CHIZA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wakulima nchini kupata zana bora, Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa pembejeo inatoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wakulima wakiwemo wa Mikoa ya Kusini kwa ajili ya kununua matrekta mapya na zana zake. Kiwango cha juu cha mikopo ni shilingi 35,000,000/= ambacho hutakiwa kurejeshwa katika kipindi cha miaka mitatu kwa riba ya kati ya asilimia 8 hadi 10.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2003/2004 hadi 2005/2006, jumla ya matrekta 96 yenye thamani ya shilingi 3,036,294,398 yamekwisha kukopeshwa kwa wakulima. Kati ya hayo matrekta 11 yamekopeshwa kwa taasisi na watu binafsi katika Mikoa ya Kusini. Kwa mfano, Dayosisi ya Anglikana, Jimbo la Masasi imepata mkopo wa matrekta matatu na zana zake yenye thamani ya shilingi 105,000,000. Dayosisi ya Jimbo Kuu la Songea, imepata mkopo wa matrekta matano yenye thamani ya shilingi 113.731 milioni ili kuanzisha vituo vya kukodisha matrekta kwa wakulima. Aidha, wakulima watatu kutoka Wilaya za Tunduru, Masasi na Songea vijijini wamepata mikopo ya kununua matrekta moja moja na zana zake. *(Makofi)*

Pia, wakulima watatu wa kutoka Madaba, Peramiho na Mahanje wamepata mikopo ya kukarabati matrekta yao na kufanya jumla ya fedha iliyokwishakopeshwa kwa wakulima wa Mikoa ya Kusini kufikia shilingi 314,999,928.

Mheshimiwa Spika kuhusu zana zinazokokotwa na wanyamakazi, Serikali imekarabati vituo 55 vya maksai katika Wilaya mbalimbali nchini. Vituo vinavyoendelea kukarabatiwa katika Mikoa ya Kusini ni Chipuputa, Lilungu, Lilambo, Utiri na Masonya. *(Makofi)*

Vituo hivi vimepatiwa zana mbalimbali na wakulima walio jirani na vituo hivyo wanaendelea kupata mafunzo juu ya matumizi ya zana bora. Jumla ya shilingi 45,662,000/= zimetumika katika kuendeleza mpango wa matumizi ya wanyamakazi katika Mikoa hiyo ya Kusini.

Aidha, vikundi 8 vyenye wakulima 210 vimefadhiliwa na mradi wa *PADEP* katika Wilaya ya Masasi na vimepatiwa zana za wanyamakazi zenye thamani ya shilingi 16,058,600/=.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wakulima wadogo wa aina hii kupata zana, Mfuko wa Taifa wa pembejeo katika mwaka 2006/2007 utaanza kutoa mikopo kwa ajili ya kununua zana zinazokokotwa na maksai kama vile plau, mikokoteni, ripa, majembe ya palizi na mafuta.

Kwa hiyo, natoa wito kwa wakulima kujiunga katika vyama vya kuweka na kukopa ili viweze kuwadhaminiwa kwa ajili ya mikopo ya aina hii.

Aidha, kwa kuwa wakulima wengi wanakosa dhamana ya mikopo, natoa wito kwa Halmashauri za Wilaya kuangalia uwezekano wa kuwadhamini wakulima wao hasa wale wenye lengo la kuanzisha vituo vya kukodisha matrekta.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa majibu mazuri. Hata hivyo, nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa mfuko wa pembejeo wa kilimo una masharti magumu kama vile kuwepo kwa dhamana ya vitu kama nyumba na kwa kuwa Halmashauri zetu za Wilaya baadhi ya Halmashauri hazina uwezo huo. Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kupunguza masharti hayo magumu ili kuwapa nafasi wakulima wengi wao wakiwa ni wakulima wadogo?

(b) Kwa kuwa kilimo bora ni pamoja na kuwepo na zana za kilimo pamoja na wataalam wa Ugani. Je, Serikali ina mpango gani wa kukifufua Chuo cha Kilimo Naliendele Mkoani Mtwara ili kiweze kuzalisha wataalam bora kwa manufaa ya Taifa kwa Mikoa ya Kusini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Njwayo kwamba masharti yale yanaonekana kidogo kuwa magumu lakini nadhani lazima tukubaliane kwamba kila kitu lazima kiwe na mahali pa kuanzia halafu tunakuwa tunaendelea kutazama jinsi tunavyoweza kulegeza masharti hayo.

Lakini nataka nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa wale wakulima ambao hawana dhamana hasa kama nyumba zisizohamishika. Tumewakubalia kujiunga katika vyama vya akiba na mikopo ambavyo vyenyewe vinaweza kudhaminiwa na Shirikisho la *SCALT* ili kuwawezesha kupata mikopo. Na baadhi ya wakulima tayari wamekwishaanza kupata mikopo kwa dhamana hii ya *SCALT*.

Lakini hata hivyo kuhusu Halmashauri za Wilaya si kweli kwamba zote hazina ubavu huo. Maana baadhi tumewashauri kwamba wafanye namna hiyo, lakini bado wanasita. Mimi bado nasisitiza kwamba Halmashauri za Wilaya pale ambapo zina uwezo zijitahidi kuwadhamini watu hawa wakati tunatafuta namna ya kupunguza masharti hayo.

Kuhusu kufufua chuo cha Kilimo cha Naliendele Mtwara. Sasa hivi vyuo vyetu tulivyo navyo, tunavyo vyuo tisa (9) na chuo hicho sasa kinatambulika kwa jina la Mtwara. Watu wa Utafiti wanatumia jina la Naliendele. Lakini kwa upande mwingine tunaita kwa mafunzo. Mtwara Chuo cha Mafunzo. Lakini ukitazama ni kwamba mpaka sasa hivi vyuo vyetu vinaendeshwa *below capacity* kwa wanafunzi waliyomo katika vyuo vyetu kama ni *full capacity* ingekuwa wanafunzi 1,670. Sasa hivi wanafunzi

walioko hawazidi 800 lakini ni kutokana na kwamba wanafunzi walio wengi wanatakiwa wajilipie na walio wengi hawawezi wakajilipia. Kwa hiyo, hivi sasa ni kwamba tuangalie kwanza hivyo vyuo vilivyopo viweze kuendeshwa *full capacity* kabla hatujaweza kuongeza gharama zingine za kuendesha mafunzo.

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba matrekta haya ni watu wachache walio nayo na katika wale waliokopeshwa Mfuko wa Pembejeo hajaligusia vyama vya ushirika ambavyo vinalelewa na Wizara yake. Matrekta yaliyokuwa yanafanya kazi Mtwara yalikuwa yanamilikiwa na vyama vikuu vya ushirika, *Masasi Mtwara Corperative Union* na *Tandahimba Newala Corporative Union.* Matrekta yale sasa yamekufa.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anaweza kutuahidi hapa katika Bunge hili kwamba kwa sababu vyama vya ushirika ni vyake anavilea yeye atashirikiana na vyama vikuu vya ushirika viwili vya Mkoa wa Mtwara kuhakikisha kwamba zinapata matrekta ili vitoe huduma kwa wakulima wake?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, vyama vya Ushirika kama inavyoeleweka hivi sasa karibu katika nchi nzima vinasuasua na sisi tunaelewa kabisa kwamba vyama vya ushirika kusuasua kwake ndiko kumeleta matatizo makubwa kwa wananchi hasa wakulima, ikiwa siyo kwa mpango wa matrekta tu ni pamoja na upatikanaji wa pembejeo na huduma zingine.

Serikali sasa hivi iko katika mpango wa kuhakikisha kwamba vyama vya ushirika vinafufuliwa na vinaboreshwa. Sasa napenda nimwahidi kama mwenyewe alivyouliza kwamba kama vyama vya ushirika vilivyopo katika mkoa wa Mtwara na mahali pengine popote Tanzania vitaonekana kuwa imara vinavyokopesheka ambavyo vinaweza kulinda maslahi ya wakulima, kama ilivyokuwa zamani. Mimi nina hakika kabisa kwamba vyama hivyo vitapata mikopo ya matrekta.

Na. 114

**Utoaji wa Mafunzo ya Kilimo**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA (k.n.y. MHE. MHONGA SAID RUHWANYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika katika msimu uliopita haikufanya vizuri kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo na upungufu wa mvua:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kutoa mafunzo ya Kilimo cha Kisasa kwa njia mbalimbali kama *Radio, Television* na Magazeti pamoja na kutoa Semina ya kilimo kwa wakulima kwa kutumia wataalam wa kilimo kutoa ujuzi kwa wakulima na

kwa kutumia ujuzi huo waweze kuzalisha zaidi katika kilimo na kurudisha mikopo ya pembejeo za kilimo wanazokopa

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwa maji ya mvua yanavunwa kwa ajili ya umwagiliaji na kwa matumizi ya mifugo katika kipindi cha ukame?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kupitia kitengo chake cha Elimu kwa Wakulima inaendelea kutumia mbinu mbalimbali za kuwafikishia wakulima ujumbe na elimu ya kilimo bora kwa lengo la kubadilisha kilimo cha kujikimu kuwa cha kibiashara na chenye tija.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kipindi cha Redio cha Mkulima wa Kisasa kipo hewani kupitia *Radio Tanzania* kila siku ya Jumatatu, kuanzia saa 11.45 hadi saa 12.00 jioni.

Wakati wa Mkutano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kipindi hiki hurushwa kuanzia saa 9.30 hadi 10.00 jioni.

Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji *(PADEP)* huandaa na kurusha kipindi cha Kilimo kila siku ya Jumamosi saa 12.45 jioni kupitia *Radio Tanzania* na kipindi cha Televisheni kupitia TVT siku ya Jumatatu saa 7.00 mchana na saa 12 jioni ambacho kinarudiwa siku ya Jumatano saa 7 mchana.

Mbinu zingine zinazotumika kuwaelimisha wakulima ni pamoja na:-

(i) Kutengeneza gazeti la Mkulima wa Kisasa ambalo linaeleza mbinu na kanuni mbalimbali za Kilimo Bora na kulisambaza kwa wakulima.

(ii) Kutengeneza vipeperushi, vijitabu na mabango yenye kanuni za Kilimo Bora na kuvisambaza kwa wakulima.

(iii) Kutayarisha na kutangaza vipindi vya redio na televisheni kuhusu kilimo na mbinu za kuboresha kilimo.

(iv) Aidha, wakulima pia wanapata stadi na maarifa ya kilimo kwa mafunzo maalum ya muda mfupi yanayotolewa kwenye vyuo vya wakulima vya Inyala, Mkindo, Ichenga na Bihawana.

Vile vile mafunzo hutolewa na Maafisa Ugani kwa wakulima katika maeneo yao kupitia mbinu shirikishi ya mashamba darasa kulingana na mahitaji ya wakulima katika maeneo yao.

(b) Mheshimiwa Spika, athari za ukame unaotokea mara kwa mara nchini ni pamoja na uhaba wa mazao ya chakula na biashara na kupoteza mifugo. Kwa kuliona hilo, Serikali inaendelea na mpango wa kujenga mabwawa ya kuhifadhi maji kwa ajili ya kumwagilia mashamba na kunywesha mifugo hasa katika Mikoa kame.

Katika mwaka 2006/2007, Serikali inafanya usanifu wa mabwawa 40 ambayo yatajengwa chini ya Programu ya *ASDP*.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa hapa Tanzania wakulima wamekuwa wanakosa ushauri wa kitaalam kutokana na kuwepo na Afisa Ugani wachache sana katika ngazi ya Vijiji, Kata na Tarafa; na kwa kuwa wamekuwepo vijana waliomaliza vyuo mbalimbali hapa Tanzania lakini wengi wao wameishia mitaani na wengine kufanya kazi tofauti na fani zao kutokana na kukosa ajira. Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba kunakuwepo na wataalam wa kutosha katika ngazi zote ili wakulima wetu waweze kuwa na ukulima wenye tija? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa hata wale Maafisa Ugani wachache walio kwenye vituo vya kazi hawaonekani wakati wanapotakiwa kutoa huduma. Wakulima wakiwafuata hawawaoni kutokana na kwamba wanajishughulisha sana na masuala yao binafsi na kuacha mbali huduma wanayopewa. Na kwa kuwa Halmashauri zetu zimekuwa hazifuatilii kuona kwamba watendaji hawa wanafanya kazi yao kikamilifu. Je, Serikali sasa ina mpango gani sambamba na kuboresha kilimo kuhakikisha kwamba wafanyakazi hawa wanatimiza wajibu wao kuweza kutoa huduma inayostahili kwa wakulima wetu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba ili tuweze kuboresha kilimo lazima tuboreshe huduma za Ugani. Kwa sababu kilimo chetu kwanza ni kilimo cha wakulima wadogo wadogo si cha wakulima wakubwa ambao wanaweza kuajiri Maofisa Ugani wao wenyewe. Kwa hiyo, wanategemea sana huduma ya ugani kutoka kwa Maofisa wa Serikali.

Kwa sababu hiyo ningependa kutumia nafasi hii kueleza ya kwamba Wizara yangu inachunguza hivi sasa juu ya mapungufu yote yaliyoko katika huduma za ugani nchini pote ili kuona ni hatua gani zinazostahili kuchukuliwa. Kama tulivyosema katika hotuba yetu wakati wa Bajeti tunashirikiana na Wizara ya TAMISEMI na tulikwishaanza kushirikiana nayo na kugundua ya kwamba mahitaji ya Maofisa wa Ugani nchini kote yanafikia jumla ya maofisa 12,000.

Lakini nchini pote tunao maofisa au watendaji kazi 3,800. Kwa hiyo hiyo unaweza ukaiona dhahiri ya kwamba kuna upungufu mkubwa sana wa Maofisa wa Ugani. Hilo labda la kwanza na mimi nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tunatazama suala hili kwa makini sana kwa sababu tunatambua hatuwezi kuboresha kilimo bila kufikisha maarifa ya sayansi ya kilimo kwa wakulima. *(Makofi)*

Na swali la pili, kwa wale ambao wapo tayari na ambao inasemekana hawaonekani. Ningependa kusema ya kwamba tutashirikiana na TAMISEMI na Halmashauri za Wilaya ili kujipanga upya kuona jinsi tunavyoweza kuwahudumia hao wakulima. Vile vile waweze kutenda kazi yao vizuri. Baadhi yao wako huko vijijini, wamekaa muda mrefu na wamepoteza wakati mwingine ile morali ya kufanya kazi kwa sababu hawana huduma zinazostahili, hawana usafiri na kadhalika. Kwa hiyo, yote tunayatazama kwa pamoja kwa nia ya kutaka kuboresha huduma hiyo ili kuongeza uzalishaji wa mazao nchini pote. *(Makofi)*

Na. 115

**Uuzwaji wa Shamba la *NAFCO-Magamba***

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imetangaza kuliuza shamba la *NAFCO-Magamba* lenye ukubwa wa ekari 12,051; na kwa kuwa zaidi ya wananchi 10,000 walikuwa wanategemea mashamba hayo; na kwa kuwa sasa Mbozi kuna shida ya ardhi:-

(a) Je, Serikali inaweza kuwaeleza Watanzania kwamba mashamba hayo yameuzwa kwa fedha kiasi gani na; je kiasi hicho ni faida au hasara?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuwatafutia wananchi hao maeneo mengine au iwaruhusu kuanzisha mashamba mapya kwa kufyeka misitu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, shamba la mahindi la Mbozi liko chini ya *PSRC* na lipo kwenye mchakato wa kubinafsishwa. Aidha, wataalam walioteuliwa na *PSRC* sasa wanaendelea kufanya upimaji na kuweka mipaka ya shamba, na kufanya uhakiki wa mali na uthamini na kuendelea kufanya uhakiki wa mali na uthamini. Kwa kuwa mchakato wa uuzaji wa shamba hili bado haujakamilika ni mapema mno kusema litauzwa kwa fedha kiasi gani.

(b) Mheshimiwa Spika, kama kawaida ya Serikali inajali wananchi wake. Hivyo, kama wananchi wa Magamba watahitaji maeneo mengine wanaweza kupewa kwa

kufuata utaratibu wa Serikali. Aidha, kutokana na umuhimu wa kuhifadhi mazingira wananchi wataruhusiwa tu kufungua mashamba katika sehemu zile tu zitakazobainika kutokuwa na athari ya mazingira na siyo kwenye hifadhi ya misitu au vyanzo vya maji.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata majibu ya Serikali kuhusu swali langu. Lakini naomba niulize Serikali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba bado mchakato unaendelea na kwamba lipo *PSRC* na kwa kuwa mimi najua kwamba wananchi wa Lushoto kule Usambara waliungana na kununua mashamba ya chai pamoja na kiwanda kile cha Mponde na kwa kuwa bado halijauzwa shamba hili. Je, Serikali haiwezi ikatumia utaratibu iliyotumia kwa wananchi wa Usambara kule Lushoto kuwauzia wananchi hawa wa Wilaya ya Mbozi ambao kwa kweli wana shinda kubwa sana ya ardhi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu uhaba wa ardhi katika Wilaya ya Mbozi, napenda niseme tena kitaalam kwamba utafiti wetu chini ya *ESDP* unatuonyesha kwamba *land pressure* katika Wilaya ya Mbozi iko kati ya asilimia 68 na 70 na kwa hiyo uhaba kabisa wa ardhi katika Wilaya ile ya Mbozi siyo wa kutisha kama katika mikoa hii ya Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye utaratibu wa kuuza mashamba haya, anavyodai Mheshimiwa Mbunge ni sawa. Lakini pia napenda nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari katika Wilaya ya Mbozi mashamba ya kahawa ya Rwanda, Ng’amba na Shiwanda tayari yameshauzwa kwa wananchi kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi. Lakini hadi hivi sasa Halmashauri ya Wilaya haijaweza kulipa hata ile asilimia 40 ambayo waliambiwa walipe kwa ajili ya mashamba haya ili waweze kuwapatia wananchi wao.

Sasa mimi nafikiri kwanza mngetekeleza haya, haya ya kahawa mliokwishapewa kupitia kwenye Halmashauri yakikamilika basi ndiyo mnaweza kujenga hoja nyingine. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa kazi ya Serikali zaidi ni kutoa huduma kwa wananchi wake na siyo kufanya biashara. Kwa mtindo huu wa kasi ya kuuza ardhi Serikali inafikiria itatengeneza sayari gani ambapo wananchi wanaozaliwa wataweza kuishi na kuweza kutumia ardhi?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, Serikali haiuzi ardhi, Serikali inauza mashamba ambayo yalikuwa yanamilikiwa na Serikali kwa wakati huo. Na kuuza shamba ni tofauti na kuuza ardhi. Shamba lazima liwe juu ya ardhi. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, Serikali inachofanya ni kwamba kuna mradi wa Serikali kama ilivyokuwa mashamba ya Kapunga. Sasa haiwezi kufanya biashara. Inasema wewe

utalima pale, unarudisha gharama zile tu ambazo ni za thamani ya huduma iliyotolewa pale kwenye shamba halafu unaendelea kulima.

Hiyo ni tofauti na Sera ya kuuza ardhi. Sheria ya Ardhi inaiweka ardhi kuwa mali ya Serikali na haiuzwi isipokuwa miradi iliyoko juu ya ardhi ina thamani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana tunaendelea. Sasa tunahamia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali linaulizwa na Mheshimiwa, samahani, ooh sawa sawa kweli. Leo yako matatu ya Kilimo, loo! Mheshimiwa Felix Kijiko, swali linalofuata.

Na. 116

**Kuendeleza zao la Pamba Mkoani Kigoma**

**MHE. FELIX N. KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa katika miaka ya 1970 kilimo cha zao la pamba kilishamiri sana Mkoani Kigoma hususan Wilaya ya Kibondo ambapo Mamlaka ya Pamba wakati huo iliamua kujenga kiwanda cha kuchambua pamba na sasa kutokana na bei ndogo ya pamba wakulima wamekata tamaa kuendeleza zao hilo:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza zao hilo Mikoani Kigoma?

(b) Je, ni nini hatma ya kiwanda cha kuchambua pamba *(Kakonko Ginnery)* ambapo hadi leo hakijaanza kufanya kazi tangu kujengwa kati ya miaka ya 1970-1980?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mhesihmiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Felix Kijiko, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Kiwanda cha kuchambulia pamba cha Kakonko kilijengwa kwa fedha za Serikali kupitia iliyokuwa Mamlaka ya Pamba. Kutokana na uhaba wa fedha, ujenzi wa kiwanda haukukamilika ikiwa ni pamoja na ufungaji wa mitambo ya kuchambulia pamba. Mwaka 1989 Serikali ilimilikisha miundombinu ya kiwanda hicho hususan maghala, nyumba za watumishi, mizani ya kupima magari kwa Chama cha Ushirika cha Buha.

Kutokana na madeni ya benki *Loan Advance Realization Trust (LART)* ilifilisi Chama cha Ushirika cha Buha na wadai wakalipwa haki zao. Baada ya muda mrefu kupita bila kupatikana mnunuzi wa kiwanda hicho kulingana na thamani yake, mwaka 2004, iliuza miundombinu ya kiwanda hicho kwa mfanyakabiashara anayejulikana kwa jina la Jamal A. Tamim wa Tarafa ya Mabamba Wilayani Kibondo kwa thamani ya shilingi milioni kumi na kufunga mahesabu kisheria. Kwa sasa Serikali inaendelea

kumfuatilia mfanya biashara huyo ili kujua mikakati yake ya kuendeleza kiwanda hicho na kufanya kazi yake iliyokusudiwa ya kuchambua pamba.

Mhesihmiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix Kijiko, Mbunge wa Muhambwe, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Pamba kwa kushirikiana na viongozi wa Wilaya inaendesha kampeni ya kufufua kilimo cha zao la pamba Mkoani Kigoma katika Wilaya za Kibondo na Kasulu. Uzalishaji wa pamba katika Wilaya hizo umeongezeka kutoka tani nne (4) katika msimu wa 2000/2001 hadi tani 697 katika msimu 2005/2006. Katika kipindi hicho, mfuko wa kuendeleza zao la pamba ulitoa mkopo wa pembejeo hususan madawa na Serikali ilihakikisha kwamba wakulima wanapata soko.

Kwa kuwa moja ya vichocheo vikubwa vya uwekezaji katika pamba ni kiasi cha pamba inayouzalishwa, Serikali inaendelea kuhamasisha wakulima wa pamba kuongeza uzalishaji kufikia angalau kilo 2,000,000 ili kuwavutia wawekezaji.

Kwa sasa tunawashawishi wawekezaji kujenga viwanda vya kuchambua pamba katika Mikoa ya Kigoma, Tabora na Singida. Mikoa mingine ni Kilimanjaro, Manyara, Tanga na Morogoro ambapo viwanda havipo kabisa au vilivyopo vimechakaa.

Mikakati mingine ni kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima mapema, kufanya kampeni ya bei nzuri, ununuzi kufanywa mapema na kuondoa vikwazo vyote vinavyowafanya wakulima wakatwe makato mengi yasiyo ya lazima ikiwa ni pamoja na udanganyifu unaoweza kufanywa na wanunuzi kwa visingizio mbalimbali.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa miundo mbinu ya *Kakonko Ginnery* ilikwishauzwa na *LART* ikafunga mahesabu kwa mujibu wa sheria, Serikali kupitia uongozi wa Mkoa wa Kigoma inaendelea kumfuatilia mfanyabiashara aliyenunua miundombinu ya kiwanda hicho ili kubaini mikakati aliyonayo ya kukiendeleza kiwanda ili kifanye kazi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majawabu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Nilitaka kujua Serikali ina mpango gani wa kujenga kiwanda kuchambua pamba Mkoani Kigoma hususan wilaya ya Kasulu na Kibondo?

Swali la pili, nilitaka kujua kama Serikali ina mpango wowote wa kutoa ruzuku ya madawa ya pamba kama ilivyo kwa zao la korosho?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu suala la kujenga kiwanda Serikali inajenga mazingira ambayo inawawezesha wawekezaji kujenga viwanda. Kwa sasa hivi suala la msingi kwa eneo la Kigoma ni kuwatia moyo wakulima na kuweka mazingira ambayo wataongeza zaidi

uzalishaji wa zao la pamba ili kuwavutia wawekezaji wa viwanda kujenga jinari katika eneo hilo.

Sasa sijui ni kipi kinachoanza ni pamba au jinari lakini nadhani tukiongeza uzalishaji wa pamba watavutiwa zaidi kuweka jineri kama walivyoweka katika maeneo mengine. Kwa hiyo, mpango tulionao ni kuhakikisha kwamba tunaweka jinari kama walivyoweka katika maeneo mengine. Kwa hiyo, mpango tulionao ni kuhakikisha kwamba tunawasaidia wakulima wa Kigoma kuongeza zao la pamba ili waweze kuvutia wawekezaji kujenga jinari katika eneo hilo.

Swali la pili kuhusu suala la ruzuku kwa zao la pamba kwamba hili tunalitazama kwa ajili ya msimu unaofuata. Lakini msimu uliopita uwezo wa Serikali ulikomea katika kutoa ruzuku ya sh. 21 bilioni. Sasa kwa kuwa hazitoshi kuweza kutoa ruzuku kwa mazao yote nchini tutatazama uwezo wa Serikali katika msimu unaokuja ili kuona kwamba mazao mengine mbali na korosho vile vile yanaingizwa katika mpango huu. *(Makofi)*

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kilimo cha pamba kinapendwa na wakulima wengi sana hapa nchini, wakiwemo wakulima wa Wilaya ya Chunya Mkoani Mbeya na kwa kuwa walitishwa wakulima hao kulima kilimo cha pamba kutokana na mashambulizi ya mdudu *American Read Ball.*

Lakini tangu wakati huo wakulima wameendelea kuhoji Serikali kwamba ni lini wataruhusiwa kulima pamba na wanatuhoji sisi viongozi wakiwemo Wabunge. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuwa na utaratibu wa kutoa taarifa za mara kwa mara kwa wakulima hawa kupitia kwa sisi Wabunge ili wakulima hao watimize dhamira yao ya kuongeza uzalishaji wa pamba na je, hali hiyo ikoje hivi sasa? Ningeomba nipate kufahamu. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali bado imesitisha kilimo cha pamba katika Wilaya ya Chunya kutokana na kuwepo kwa mdudu funza anayeitwa *American Read Ball* mwenyewe kama alivyosema. Kinachoendelea kufanyika hivi sasa kama nilivyokwisha jibu huko nyuma ni kwamba wataalam wanaendelea kufanya utafiti wa jinsi ya kumdhibiti mdudu huyu.

Mheshimiwa Spika, tatizo ni kwamba utafiti unafanywa kwa muda mrefu. Hauwezi ukafanywa kwa siku moja kwa sababu ni lazima uangalie ni hatua gani utakazozichukua kuweza kudhibiti kwamba huyu dudu kabisa utamwangamiza. Tatizo lingine lililopo ni kwamba ili kumdhibiti mdudu huyu inabidi kutumia madawa. Sasa wataalam wetu wa Wizara ya Kilimo wanaangalia gharama zinazohitajika kutumia madawa kumdhibiti mdudu funza huyu ni kiasi gani ukilinganisha na gharama za uzalishaji wa pamba hiyo. Kwa kuwa huu utafiti bado unaendelea naomba wakulima wa Wilaya ya Chunya waendelee kuvumilia mpaka utafiti utakapokamilika ili tuweze

kuwapa majibu ambayo ni sawasawa. Hivi sasa tukiruhusu kwamba waanze kulima tutakuwa tumeruhusu mdudu funza kuenea katika mikoa yote inayolima pamba na tutaleta hasara kubwa sana katika Tanzannia.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Naibu ametueleza kwamba Bodi ya Pamba ndiyo iliyojenga miundombinu kwa nia ya kuweka jineri pale Kakonko. Na miundombinu hiyo imekaa kwa zaidi ya miaka 10 bila kutumika hivi Serikali inawaambia nini wananchi wa Mkoa wa Kigoma ambao walichangamkia sana kulima zao la pamba lakini kumbe Bodi ilikuwa haijajiandaa kupata mitambo ya kuweka pale kwa maana hiyo Serikali imefifiza juhudi za wananchi wa Kigoma katika kulima zao la pamba?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, historia ya zao la Pamba, inaonyesha ya kwamba kuna wakati ambapo kwa kweli imefifia sana katika miaka ya hivi karibuni, siyo katika mkoa wa Kigoma peke yake lakini hata katika eneo linalolima Pamba kwa wingi katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, takwimu za uzalishaji wa zao la pamba, zinaonyesha ya kwamba Pamba ilishuka uzalishaji mpaka ikafikia marobota 190,000 kutoka marobota 500,000 ambayo ndiyo ilikuwa-*record* ya huko nyuma. *(Makofi)*

Kwa hiyo, matatizo ya zao la pamba, hayakutokana na kushindwa kujenga *Ginnery*. Hata kule ambako *Ginnery* zilikuwepo bado zao la Pamba lilishuka.

Kwa hiyo, ninachoweza kusema hapa ni kwamba tujitahidi kuongeza uzalishaji wa Pamba katika Mkoa wa Kigoma, ili tushirikiane na uongozi wa Mkoa wa Kigoma na wawekezaji, kurekebisha hali ili tuweze kuanza kuona uzalishaji unaongezeka.

Mheshimiwa Spika, lakini nia ya Serikali wakati ule ya kujenga *Ginnery* Kigoma ilikuwa nzuri. Lakini matatizo ya kiuchumi ndiyo yaliyoifanya hali hiyo ikawa ilivyo na sasa kuhoji hayo mambo ya kwamba nani alifanya nini, haitusaidii. Kitakachotusaidia kwa sasa ni kuweka mikakati itakayosaidia kuongeza ubora na uzalishaji wa pamba katika mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Na. 117

***Dual Citizenship***

**MHE. DR. ALI TARAB ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa wapo Watanzania wengi waishio nchi za ng’ambo kwa kipindi kirefu sasa na kwamba wangependa wapate manufaa *(benefits)* wapewayo raia wa nchi hizo kwa kuchukua Uraia wa nchi waishizo bila ya kupoteza Uraia wa nchi yao ya Tanzania:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati wa kuwaruhusu wananchi wetu kama hao kuwa na Uraia wa nchi mbili *dual cetizenship?*

(b) Je, Taifa letu litaathirika vipi ikiwa litaruhusu Watanzania kuwa na Uraia wa nchi mbili?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hivi karibuni umeibuka mjadala kuhusu uraia wa nchi mbili *(dual citizenship).* Wapo wanaopendekeza Serikali iruhusu watu wake kuwa na uraia wa nchi mbili lakini wako pia wengine wanaopinga hoja hiyo. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania pamoja na Sheria ya Uraia Namba 6 ya mwaka 1995, ikisomwa pamoja na Kanuni zake za mwaka 1997, uraia wa nchi mbili unaruhusiwa tu kwa watoto walio chini ya umri wa miaka 18, ambao hata hivyo wanapaswa kuukana uraia wa nchi nyingine wanapofikisha miaka 18. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na faida ambazo nchi yetu au raia wa nchi hii wanaweza kupata kutokana na kuwa na uraia wa nchi nyingine bila kupoteza uraia wa Tanzania, Serikali imechukua hatua kwa kuielekeza Tume ya Kurekebisha Sheria pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria kukusanya maoni kwa wadau mbalimbali ili Serikali ifanye uamuzi kuhusu suala hili.

Aidha, Wizara yangu ipo katika mchakato wa kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusiana na suala hili. Baada ya Waraka huo kujadiliwa na kufanyiwa uamuzi Serikali itatoa taarifa rasmi kuhusu suala la uraia wa nchi mbili.

(b) Mheshimiwa Spika, uraia wa nchi mbili unaweza kuwa na madhara ya kiusalama na kiuchumi kama utatumiwa vibaya kama vile kufanya mambo ya ujasusi. Aidha, kwa kuwa raia wa nchi yetu na nchi nyingine halazimishwi kuchangia kuchumi katika maendeleo yanchi yetu. Upo uwezekano wa kutumia faida ya kuwa Mtanzania kuifanya nchi hii kuwa mahali pa kuchumia na siyo kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mjadala ulioibuka juu ya jambo hili, imeamuliwa mapendekezo ya Tume ya Kurekebisha Sheria yapelekwe Baraza la Mawaziri kwa uamuzi ili uwepo msimamo rasmi wa Serikali kuhusu jambo hili. *(Makofi)*

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, je, hatuoni kwamba kuruhusu mpango huu tunaweza kufaidika kwa kupata wataalam ambao tunawahitaji. Madaktari, Walimu, Wahandisi na pengine hata kupata wawekezaji, kwani raia wetu walioko nje wakifaidika kipato chao wanakirejesha nyumbani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msinigi suala hili bado linafanyiwa kazi. Serikali inafahamu kwamba faida zinaweza zikawepo. Lakini pia kama nilivyoeleza hasara pia zinaweza zikawepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tungependa Mheshimiwa Mbunge avute subira, Serikali ifanyie kazi suala hili na baadaye tupate nafasi ya kutoa tamko letu rasmi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Serikali inasema jambo hili linaandikiwa Waraka. Mimi nadhani tuendelee. *(Makofi)*

Na. 118

**Ufinyu wa Magereza Nchini**

**MHE. MOHAMED ALI SAID** aliuliza:-

Kwa kuwa msongamano wa wafungwa katika magereza nchini ni mkubwa sana na kwa kuwa kuna magereza 122 nchini ambayo yanaruhusiwa kuhifadhi wahalifu 22,669 lakini hivi sasa yanahifadhi wastani wa wahalifu 45,000 na kwa kuwa takriban nusu ya hao ni mahabusu ambao kesi zao hazijaamuliwa na Mahakama:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za kuondoa tatizo hilo kwa haraka sana?

(b) Je, kwa kushindwa kufanya marekebisho ya kuongeza majengo kwa haraka, Serikali haioni ni vema mahabusu kupunguza msongamano katika magereza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Ali Said, nadhani kwa Bunge hili ni mara ya kwanza unauliza au? Hongera sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Ali Said, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba upo msongamano mkubwa kwa baadhi ya Magereza yetu nchini ambapo idadi halisi ya wafungwa na mahabusu katika magereza hayo ni mkubwa kuliko uwezo kisheria wa magereza hayo huhifadhi wahalifu ambao ni eneo lisilopungua futi za mraba thelathini kwa mfungwa mmoja.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza limepewa kisheria jukumu la kuwapokea na kuwahifadhi wahalifu wote wanaoletwa na mamlaka zinazoruhusiwa kisheria kuwapeleka wahalifu gerezani ili mradi ipo hati maalum iliyotolewa na mamlaka hizo husika. Magereza hawaruhusiwi kisheria kuwaachilia wahalifu hao mpaka itolewe hati nyingine ya kuwaachilia kutoka gerezani.

Hatua ambazo zimekuwa zikichukuliwa na Serikali kupunguza msongamano wa wahalifu magerezani ni kama ifuatavyo:-

(i) Kila inapowezekana Polisi kukamilisha upelelezi kabla ya kumkamata mtuhumiwa ili mara baada ya kumkamata kesi ianze.

(ii) Kuhimiza uharakishaji wa upelelezi na uendeshaji mashauri kupitia Kamati za Kusukuma Mashauri yaani *Case Flow Management Committees* katika ngazi ya Wilaya na Mkoa.

(iii) Kuanza mchakato wa kutenganisha shughuli za upelelezi *(investigation)* na uendeshaji wa mashauri mahakamani *(prosecution)* kwa lengo la kuharakisha upelelezi.

(iv) Kupanua na kuongeza magereza ya mahabusu *(Remand Prisons)* ambayo awali yalijengwa kwa ajili ya wahalifu wachache lakini kutokana na uhalifu kuongezeka yamelazimika kuhifadhi wahalifu kupita uwezo wake.

(v) Ukarabati wa magereza ya zamani kwa kuimarisha mabweni ambayo yalikuwa hayatumiki kutokana na uchakavu na hivyo kutokuwa imara kiulinzi kuhifadhi wafungwa na mahabusu.

(vi) Kuendeleza ujenzi wa Magereza ya Mahabusu *(Remand Prisons)* mapya katika Wilaya ambazo hazina magereza ya mahabusu.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba suala la mahabusu kupewa dhamana ili wabakie nje kama njia ya kupunguza msongamano katika magereza yetu ni la msingi, utoaji wa dhamana pamoja na kuwa ni haki ya mshtakiwa, hutegemea zaidi uamuzi wa mahakama kwa kuzingatia shauri lililo mbele yake.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo hili la msongamamo wa mahabusu Magerezani ni kubwa na watu wengi wanalilalamikia; na kwa kuwa msingi wake mara nyingi inakuwa ni hoja wanaoshtaki ni kwamba hawajakamiliisha ushahidi. Serikali inaonaje ikatoa muda maalum kwa askari wanaoshtaki, kuwa ukipita muda fulani hamjakamilisha basi inapaswa kesi hii kufutwa ili kuharakisha mambo haya. Kwa sababu hata kesi ya kuiba kuku tu kwa nini inakaa miezi mitatu mpaka minne, ushahidi haujapatikana? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba wakati mwingine upelelezi unachelewa hali ambayo inasababisha msongamano ndani ya mahabusu kuongezeka. Lakini pia ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge, kwamba Wizara yangu pamoja Wizara ya Katiba na Sheria, pamoja na Wizara ya Usalama wa Raia, tunafanya kazi kwa pamoja hivi sasa kuhakikisha kwamba mashauri ya watuhumiwa ambao wako katika mahabusu ya Tanzania, zinapelekwa haraka zaidi kwa kuangali aina ya kesi iliyoko Mahakamani, ili kuhahakisha kwamba msongamano unapungua.

Ningependa kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba suala la kusema kwamba tuwaachie wafungwa wa mahabusu, kwa sababu muda umepita inaweza isiwe nzuri sana kwa sababu wengine hawa ni wahalifu. Hatuwezi kuruhusu wahalifu kutoka nje kwa sababu tu muda wa kusikiliza kesi umekuwa ni mrefu. Lakini ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali, tatizo imeliona tunalifanyia kazi na tutajitahidi

kadri ya uwezo wetu kupunguza msongamano ambao uko ndani ya mahabusu zetu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, Wizara zetu hizi tatu, Usalama wa Raia, Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Katiba na Sheria, tayari tumeshaanza kuchukua hatua na imekuwa ikijitahidi sana kupunguza idadi ya mahabusu kwenye jela zetu. Lakini tunapowapunguza na kwa sababu uhalifu uko mwingi basi wanaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, tutajitahidi kuendeleza jitihada ambazo tayari zimeishaanza ili tuone kwamba mahabusu hawajazi jela zetu. Lakini jambo kubwa ni kuongeza idadi ya jela na hapo hapo kuwaomba wananchi wa Tanzania ili Watanzania kupunguza uhalifu kusudi siku moja Magereza yetu yawe hayana wahalifu. *(Makofi)*

Na. 119

**Mradi wa Upendeleo Kuendeleza Mkoa wa Manyara**

**MHE. DORAH H. MUSHI (k.n.y. MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina mikakati mizuri ya kuwawezesha wananchi hususan wanawake kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuwapatia mikopo ya kufanyia biashara ndogo ndogo; na kwa kuwa Mkoa mpya wa Manyara una matatizo mengi makubwa ya mazingira ya kufanyia biashara hizo ikiwa ni pamoja na elimu ya ufahamu, kero za maji, uhaba wa Zahanati kwa baadhi ya vijiji na kutokuwepo na hospitali ya Mkoa.

(a) Je, Serikali ina mipango gani ya upendeleo kwa Mkoa wa Manyara ya kuboresha Mazingira chini ya Mpango wa MKUMBITA?

(b) Je, Serikali itafikisha lini mradi wa *SELF* Mkoani Manyara ikizingatiwa kuwa hakuna taasisi za fedha zinazofikisha huduma huko zaidi ya *SACCOS* zilizoanza hivi karibuni?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kimsingi maboresho ambayo yanafanyika chini ya Programu ya MKUMBITA yaani programu ya kuboresha mazingira yana lenga katika kuboresha biashara na uwekezaji kwa nchi nzima na wala sio mkoa mmoja mmoja kwa upendeleo. Hata hivyo Serikali inatambua kuwa kuna maeneo na mikoa inayohitaji kupewa kipaumbele kwa kuwa iko nyuma kimaendeleo ikilinganishwa na mikoa mingine. Mikoa hiyo ni pamoja na mkoa wa Manyara. Pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara, Serikali kupitia Wizara na asasi mbali mbali inajitahidi kuondoa kero zinazoukabii mkoa wa Manyara ambazo zimebainishwa na Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Aidha, Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji katika sekta za madini, utalii kilimo na ufugaji, fursa ambazo zinaweza kutoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya mkoa wa Manyara na Taifa zima kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Wizara itashirikiana na uongozi, watendaji na wananchi wa Mkoa wa Manyara, kufanikisha Mkutano wa Mashauriano kuhusu Uwekezaji yaani *Investors Consultative Forum* ambao unatarajiwa kufanyika mapema mwaka ujao. Shabaha ya Mkutano huu ni kutangaza fursa za kibiashara na uwekezaji za Mkoa wa Manyara na hivyo kuwavutia wawekezaji kuja kuwekeza huko. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, Mradi wa *SELF* unatarajia kuanza shughuli zake mkoani Manyara wakati wa Awamu ya Pili wa Mradi unaotarajia kuanza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, katika Awamu ya Kwanza Mradi wa *SELF* ulianza katika mikoa sita kwa majaribio na baadaye kuendelezwa hadi kufikia mikoa 14 mwaka 2004. Aidha, lengo la *SELF* ni kuifikia mikoa yote Tanzania Bara na Zanzibar kadri upatikanaji wa rasilimali (fedha) utakavyoruhusu.

(c) Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Martha Umbulla, kwa jitihada zake za kuhimiza *SACCOS* na kusaidia katika upatikanaji wa mikopo midogo midogo kwa ajili ya wanawake. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwapa shime Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuwaandaa na kuwahamasisha wananchi ili waweze kuanzisha na kujiunga kwenye *SACCOS* kwani miradi ya *SELF* inapitisha mikopo yake kupitia kwenye *SACCOs* na Asasi ndogo ndogo za fedha.

Aidha fedha za mfuko wa uwezeshaji zile bilioni moja kwa sehemu kubwa zitapitia *SACCOS* za wananchi na vikundi vya ushirika, hivyo ni muhimu kuhamasisha uanzishwaji wa *SACCOS* kote nchini. *(Makofi)*

Na. 120

**Kujenga Shule na Vyuo Vya *VETA* Mkoani Lindi**

**MHE. FATMA A. MIKIDADI** aliuliza:-

Kwa kuwa moja ya matatizo ya Mikoa ya Kusini ni kutokuwa na shule za kutosha za msingi, sekondari, Vyuo vya Elimu ya Juu na Vyuo vya *VETA* pamoja na kuwa na sera ya Taifa inayotaka kuwan a Vyuo vya *VETA* kila Mkoa: -

(a) Je, Serikali haioni kuwa huu ni wakati muafaka wa kusaidia Mkoa wa Lindi kuongeza nguvu katika ujenzi wa shule za sekondari ambapo wananchi wameshaanza kujenga kwa kujitolea na sasa wameshajenga maboma ya shule zipatazo 78?

(b) Je, Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Lindi kitajengwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua na kuuthamini mchango wa wananchi wa Mkoa wa Lindi katika ujenzi wa vyumba vya madarasa na nyumba za walimu, na kwa kuzingatia kuwa Mkoa wa Lindi ni miongoni mwa Mikoa isiyo na shule za kutosha, kwa mwaka 2006/2007 Mkoa umepewa ruzuku ya maendeleo kupitia *MMES* ya jumla ya shilingi 1,234,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 92, nyumba za walimu 59, maktaba moja, maabara mbili na hosteli ya wasichana moja.

(b) Mheshimwia Spika, ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Lindi utaanza rasmi baada ya kukamilika kwa taratibu za kumpata mkandarasi. Mkataba kwa ajili ya kupata huduma za ushauri *(Consulting Services)* wa ujenzi ulitiwa saini kati ya *VETA* na Kampuni ya usanifu ya Korea iitwayo *MAC Architecs Consultants* tarehe 24 Agosti, 2006. Kazi inayoendelea hivi sasa ni ukamilishaji wa michoro pamoja makabrasha ya zabuni *(Tender Documents).* Taratibu za kumtafuta mzabuni wa ujenzi *(bulding contractor)* zinatarajiwa kuanza mwezi Januari, 2007 na kukamilika mwezi wa Machi, 2007. Hii ni kutokana na utaratibu au taratibu za kumpata mzabuni wa ujenzi zinazofuata sheria za Kikorea kwa mjibu wa Mkataba. *(Makofi)*

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba katika nchi zote zilizoendelea, moja ya sababu ya kuendelea ni kuwa na shule ya ufundi kwa sababu wananchi wake wanajitegemea na hivyo kukuza uchumi. *(Makofi)*

Sasa tukirudi Tanzania ya Lindi karibuni 45% ya vijana wake baada ya kumaliza darasa la saba huenda katika miji mbalimbali kutafuta ajira hasa Dar es Salaam. Hivyo kukumbana na jina linaloitwa Wamachinga na kuwa usumbufu kwa wananchi, sasa nani alaumiwe? Si hivyo tu kwamba katika *speed* ile ya ujenzi wa *VETA*, takriban sasa ni miaka mitatu tangu ujengewe uzio uwanja ule. Kwa *speed* hii tunaweza tukafika mbali? Sera ya miaka mitano ya ujenzi wa *VETA* kwa kila Mkoa tutafika mbali? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niongeze kwa maelezo mazuri aliyotoa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kutokana na swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Lindi kama hivi ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Lindi kama alivyoeleza katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba kweli una mahitaji maalum na ndiyo maana kama alivyosema katika jibu la msingi kwamba mmepewa upendeleo maalum wa kiwango cha fedha kilichopatikana kwa mpango wa *MMES* kwa mwaka huu. Lakini pia ningependa kuchukua nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Fatma Mikidadi kwamba Chuo cha Ufundi Mkoani Lindi kitajengwa na kama alivyojibu katika swali la msingi ni kwamba ndani ya Mkataba wa Serikali ya Tanzania na Serikali ya Korea, ni kwamba Mkandarasi, wataalam wa usanifu wote watapatikana Korea, kwa hiyo sisi kama Serikali ya Tanzania tunasubiri taratibu hizo zikamilike huko huko Korea, kufuatana na mkataba ulivyosema.

Mheshimiwa Spika, ninachokuomba Mheshimiwa Mbunge ni kwamba tuvute subira, cha msingi ni kwamba chuo hicho kitajengwa. Lakini pia ningependa kuchukua nafasi hii kutoa wito kwa wenzetu wananchi wa mkoa wa Lindi. Kuna Chuo kizuri sana Mtwara ambako ni jirani kabisa, bahati nzuri mimi nimeshafika Chuoni hapo, ni kikubwa sana kiko Mtwara na kwa ada ni shilingi 90,000/= kwa mwaka. Ukiangalia vifaa vilivyoko Mkoa wa Mtwara kwenye Chuo cha Ufundi, nawaomba wananchi tutumie chuo kile. Mimi nimetembelea juzi tu, ilikuwa tarehe 12 Oktoba, 2006, katika chuo kile cha Mtwara. *(Makofi)*

Kwa vifaa vilivyopo pale na ukubwa wa Chuo hakitumiki ipasavyo. Ninatoa wito kwa wananchi tutumie vyuo vya ufundi vinatafuta vijana wa kujiunga pale. Ukiangalia shilingi 90,000/= na vifaa, pia ufundi wanaoupata, ninawasihi wananchi wa Lindi tutumie kituo cha Ufundi cha Mtwara. Hali kadhalika wananchi wa Mtwara wenyewe. Dereva anapatikana mzuri kabisa kwa kipindi cha mwezi mmoja tu na vifaa vilivyoko pale ni vizuri sana kutoka Japan, ninawasihi mtumie chuko kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba kumalizia kwa kuwapa moyo Watanzania kwamba Wizara ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi, inaanda mpango mzuri ambao tuna matumaini ifikapo mwaka 2010 kila Wilaya itakuwa na Chuo cha Ufundi. Lakini tutumie vilivyopo. Ahsante sana *(Makofi)*

**SPIKA:** Ila Mheshimiwa Waziri usisahau na Urambo pia. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 121

**Mitambo ya Mawasiliano - Buchosa**

**MHE. ERNEST G. MABINA (k.n.y. MHE. SAMUEL M. CHTALILO)** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Bushosa wanapenda sana maendeleo; na kwa kuwa Kampuni ya *Celtel* iliweka mnara mmoja makao makuu ya Jimbo hilo:-

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba mnara huo una uwezo mdogo wa kusambaza mawasiliano?

(b) Je, Serikali iko tayari kuiagiza Kampuni hiyo kuweka minara mingine katika maeneo ya Mwangika, Busenge, Kata ya Kazunzu, Zilagola, Maisome pamoja na Kome Kisiwani?

(c) Kwa kuwa Kampuni ya *Mobitel (tiGO)* iliingia mkataba wa kujenga mnara mmoja wa simu katika kijiji cha Nyakarilo na kuonyesha nia hiyo lakini ghafla hawakuendelea, je, ni sababu zipi zilisababisha wasiendelee; na je, Kampuni hiyo iko tayari kushitakiwa na wananchi wa eneo hilo kwa kuwalaghai?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimwia Samuel Mchele Chitalilo, Mbunge wa Buchosa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kwamba mnara huo una uwezo mdogo wa kusambaza mawasiliano na unahitajika kupanua uwezo wake. Kwa msingi huo, Serikali inaendelea na juhudi za kuzishawishi Kampuni zote husika ili vivutike kufunga mitambo yenye kuogeza nguvu na uwezo wa mnara kusambaza mawasiliano kwa wananchi walio wengi. Hatua hiyo ya kuzishawishi kampuni inakwenda sambamba na dhamira ya kuchangia *(facility sharing)* minara badala ya kila kampuni kujenga mnara wake ili kutunza mazingira.

(b) Serikali imefanya mawasiliano na *Celtel (T) Ltd.* kuhusu mpango wa uwekaji wa minara katikamaeneo yaliytajwa ambayo hayajafanyiwa tathmini bado kujua uwezo wa soko la mahitaji na tija. *Celtel (T) Ltd.* ina mpango wa kufanya tathmini katika maeneo yaliyotajwa na kuyajumuisha kwenye *Business Plan* yake kwa utekelezaji pindi fedha zitakapopatikana.

(c) Kuhusu Kampuni ya *Mobitel (tiGO)* kuingia mkataba wa kujenga mnara mmoja wa simu katika kijiji cha Nyakarilo, napenda kuchukua nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa mnara ulioahidiwa ulikwishajengwa katika eneo la Nyamazugo kijiji cha Nyakarilo na hivi sasa wananchi wa maeneo hayo wanapata huduma ya mawasiliano vizuri. Kuchelewa kwa ujenzi kulitokana na uhaba wa fedha za kutekelezea mradi huo.

(d) Aidha, *tiGO* pia wamefanya tathmini ya kujenga minara mingine miwili zaidi katika kisiwa cha Kome na Kasunzu ambayo ujenzi wake utakamilika mwezi Februari, 2007 kwa kisiwa cha Kome na Agosti, 2007 kwa Kasunzu. *(Makofi)*

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mawasiliano imedhihirika kwamba ndiyo njia nzuri ya kuweza kuzuia ujambazi. Eneo lililotajwa la Jimbo la Buchosa, lina visiwa vingi katika Ziwa Victoria, kwa mfano kama Nyamango, Zilagula, Isozu na Rubondu ambayo ni Hifadhi ya Taifa. Sehemu hizo zina ujambazi mkubwa. Je, Serikali inasema nini angalau iweke mnara katika kisiwa kimojawapo katika Ziwa Victoria? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, nakubalina na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna umuhimu mkubwa sana wa mawasiliano hasa katika kuzuia ujambazi kwenye maeneo ambayo hayafikiki kirahisi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, Wizara yangu inaendelea kuhamasisha na kuwasisitiza Makampuni haya ya simu yaweze kuweka minara kwenye maeneo aliyoyataja ikiwa ni kwenye visiwa hivyo, na ndiyo maana nimetaja kwamba Kampuni ya *tiGO* tayari ina mpango kunako mwaka 2007 kuweka minara katika kisiwa cha Kombe pamoja na kisiwa cha Kasunzu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jitihada hizi za kuhamasisha Makampuni haya zitaendelea ili visiwa vyote alivyovitaja viweze kuwekewa minara katika miaka michache ijayo. *(Makofi)*

Na. 122

**Barabara ya Mombo - Lushoto**

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Mombo - Lushoto ni ya milimani na ni nyembamba yenye kona nyingi na kwa kuwa, barabara hiyo inatumiwa na magari mengi na makubwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuipanua barabara hiyo kwa kuichonga ili kuongeza usalama wa vyombo na watu wanaotumia barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mbunge wa Lushoto, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ya Mombo - Lushoto ina jumla ya kilometa 32. Barabra hii inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS).* Ni kweli barabara hii kama zilivyo barabara nyingine zinazopita milimani ina kona nyingi na nyembamba hasa sehemu zenye miamba mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara hii ilijengwa kwa kiwango cha lami mwaka 1984 na kukamilika mwaka 1998 kwa msaada toka Serikali ya Ujerumani *(FRG)* kuptitia kwa shirika lake la Misaada *KfW.* Lengo kubwa lilikuwa ni kuboresha usafiri wa wananchi na mazao mbalimbali yanayopatikana Lushoto ikiwa ni pamoja na chai, viazi mviringo, mboga za kila aina matunda na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya melezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwezo mdogo wa kifedha kwa sasa hivi, Serikali haina mpango wa kupanua barabara yote. Serikali inaipa kipaumbele barabara hii kwa kuifanyia matengenezo ya kawaida ya kila mwaka na matengenezo ya muda maalum kwa kuweka tabaka la lami kwa sehemu zile ambazo lami imeanza kuisha *(resealing works).*

Hata hivyo kwa sehemu za barabara hii ambazo ni nyembamba sana. Serikali itaendelea kutafuta fedha toka yanzo mbalimbali ili kuzipaunua. Aidha, Wizara yangu kwa kutumia Wakala wa barabara Mkoa wa Tanga inaendelea kuweka alama za barabara na ambazo zinaongeza usalama wa barbara kwa watumiaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ningependa kutoa wito kwa madereva wanaotumia barabara hii kuendesha kwa uangalifu mkubwa ili kuepuka ajali zinazoweza kutokea kutokanana ufinyu na kona nyingi za barabara hii. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alishuhudia mwenyewe tarehe 10/10/2006 alipokuja ziarani na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba barabara za mazingira ya Lushoto inabidi zitazamwe kwa aina ya peke yake.

Sera sasa isieleze tu kwamba barabara za lami Taifa, barabara za changarawe Mkoa. Kwa Wilaya ya Lushoto tungeomba kwa kweli barabara zake ziwe za changarawe, kwa sababu barabara ya lami ile ikiwa peke yake na huko kwingine ni vumbi usafiri unakuwa ni mgumu sana.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli nilishuhudia mwenyewe hali ya barabara za Lushoto wakati nikiandamana na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ziara tuliyoifanya hivi karibuni na nakubaliane naye kwamba kwa mazingira ya Lushoto yenye milima kuna haja ya kuangalia namna ya kushughulikia barabara zile zilizoko milima siyo Lushoto tu, lakini katika maeneo mengine yote yenye milima kama Same na kadhalika.

Kwa hiyo, Serikali itaendelea kwa kweli kuangalia hali za barabara kutegemea na mazingira halisi ya maeneo husika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kidogo ili kufidia muda wa mambo mengine yaliyotangulia hapa. Kwa hiyo, tunahamia Wizara ya Fedha. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini. *(Makofi)*

Na. 123

**Kuporomoka kwa Thamani ya Shilingi**

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA** aliuliza:-

Kwa kuwa hali ya uchumi wa Tanzania imeendelea kuimarika katika nyanja mbalimbali; kwa mfano kasi ya ukuaji wa uchumi imeongezeka toka asilimia 4.0% mwaka 1998 mpaka asilimia 6.8% mwaka 2005, mfumuko wa bei umeendelea kushuka toka asilimia 12.8% mwaka 1998 mpaka asilimia 4.8% mwaka 2005.

Viwango vya riba za mikopo katika benki vimekuwa vikiteremka japo kwa kasi ndogo na riba kwa amana za wateja katika mabenki zimeonyesha kupanda kwa kasi ndogo; na kwa kuwa akiba ya nchi ya fedha za kigeni imeendelea kuongezeka kiasi cha kufikia kiwango cha kukidhi mahitaji ya nchi ya kulipia bidhaa zake zote nchi za nje kwa kiwango cha zaidi ya miezi saba:-

(a) Je, kwa nini Benki Kuu ya Tanzania haionekani kutumia akiba kubwa ya fedha za kigeni kwa kuingilia katika soko la fedha za kigeni ili kupunguza kasi ya kuporomoka kwa thamani ya shilingi yetu?

(b) Je, Benki Kuu inaweza kutoa tathmini ya faida na hasara za kuiachia shilingi ya Tanzania kuendelea kupoteza thamani yake katika soko la fedha za kigeni?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB**) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, baada ya kupitishwa kwa sheria ya kulegeza masharti ya biashara ya nje mwaka 1992, thamani ya shilingi ya Tanzania inaamuliwa na mahitaji katika soko huria la fedha za kigeni. Kwa hiyo, si Serikali wala Benki Kuu inayoweza tena kuamua kiwango cha ubadilishaji wa shilingi kwa fedha za kigeni kama ilivyokuwa ikifanyika miaka ya nyuma. Hata hivyo, Benki Kuu hufuatilia kwa makini mwenendo wa soko la fedha za kigeni kila siku ili kuhakikisha kuwa uuzaji na ununuzi unafuata misingi na taratibu zilizowekwa na pia kuchukua hatua zinazostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu huingia katika soko hilo kama muuzaji au mnunuzi wa mwisho *(buyer or seller of last resort)* pale tu inapotokea kuwa kuna mabadiliko makubwa ya thamani ya shilingi yasiyoambatana na hali na mwenendo halisi wa uchumi yaani *economic fundamentals.* Kwa mfano, mwaka 2004, iliuza kwenye soko la dola za Kimarekani milioni 319.6 na kununua kutoka kwenye soko dola za Kimarekani milioni 71.92. Mwaka 2005 iliuza dola milioni 200.3 na kununua dola milioni 23.59.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi niliyoieleza, Benki Kuu haiwezi kutumia fedha za kigeni kuzuia kuporomoka kwa thamani ya shilingi kunakofungamana na hali halisi ya uchumi. Akiba ya fedha za kigeni inatakiwa itumike wakati wa shida kama vile sasa kulipia gharama kubwa ya kununua mafuta nchi za nje ili kukabiliana na tatizo la upatikanaji umeme wa kutosha na vilevile kutokana na ukame.

(b) Mheshimiwa Spika, kushuka au kupanda kwa thamani ya fedha ya nchi yoyote ile kunaweza kuwa na manufaa au hasara. Kuporomoka kwa thamani ya shilingi ukilinganisha na dola kuna faida, hasa ikiwa kunafungamana na hali halisi ya uchumi, kwani kunasaidia kukuza mauzo yetu nchi za nje na kurejesha uwiano mzuri kati ya mauzo yetu nchi za nje na manunuzi yetu kutoka nchi za nje. *(Makofi)*

Kwa upande mwingine shilingi yenye nguvu hushawishi uagizaji bidhaa toka nje, huua viwanda vyetu vya ndani kutokana na bei nafuu ya bidhaa za nje na hudidimiza uuzaji wetu wa bidhaa nchi za nje na hivyo kumwathiri mkulima wa

mazao ya biashara. Hata hivyo, shilingi yenye nguvu ni nguzo muhimu kwa uwekezaji hasa wakati malighafi inatoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuporomoka kwa thamani ya shilingi hivi karibuni kumetokana na manunuzi yetu kupanda ghafla kutokana na bei kubwa ya mafuta ya petroli. Kwa miaka miwili iliyopita manunuzi yetu nchi za nje yamekuwa yakiongezeka kwa asilimia 25 kwa mwaka, wakati mauzo yetu nchi za nje yamekuwa yakiongezeka kwa asilimia nne tu kwa mwaka.

Hata hivyo, fedha zetu za kigeni zimebaki katika kiwango kile kile cha dola za Marekani shilingi bilioni 2 ambacho ni kiwango kikubwa, hata baada ya kulipia manunuzi makubwa ya mafuta na bidhaa nyingine kutoka nchi za nje. Fedha za misaada na mikopo kutoka kwa wahisani mbalimbali zimesaidia kufanikisha hili pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Benki Kuu inafuatilia kwa umakini suala la thamani ya shilingi na panapohitajika kuchukua hatua zinazostahili ili kuhakikisha kuwa hali hii haiathiri uchumi wetu. Pale ambapo kunakuwa na sababu za msingi *(economic fundamentals)* kama nilivyoeleza hapo awali, Benki Kuu huishauri Serikali hatua za kuchukuliwa ili kurekebisha hali hiyo. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha uchumi ambazo zitachangia kuimarisha thamani ya shilingi.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:**Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, nikubali kwamba nimeridhika kwa kiasi kikubwa na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Sasa swali la nyongeza la kwanza kwa nini Serikali imekuwa inaruhusu baadhi ya Taasisi na Makampuni hapa nchini kudai malipo kwa fedha za kigeni? Hili ninaliuliza kwa sababu ndiyo chanzo cha kuongeza mahitaji makubwa ya fedha za kigeni na kuleta *pressure* kwenye *exchange rates. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, pamoja na majibu mazuri kama nilivyosema ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, kuporomoka kwa thamani ya shilingi kunalifanya hata zoezi zima la kufanya bajeti hapa nchini linakuwa gumu. Kwa sababu unabajeti wakati dola moja ikiwa mathalan ni sawasawa na shilingi 1,100 kwa mfano, lakini leo hii dola moja ni sawasawa na shilingi 1,300 hapo tayari bajeti imekwishakuwa nje ya vile ilivyokadiriwa. Bado tunaambiwa tunayo akiba kubwa ya fedha za kigeni. Akiba kubwa ya fedha za kigeni ni pamoja na kusaidia kuwa kama mto, *cushion, exchange rate* inapoingia katika matatizo haya ambayo yanajitokeza. Swali langu la msingi lilikuwa kwa nini Benki Kuu inaendelea kuzishikilia hizi fedha kama akiba wakati thamani ya shilingi inaporomoka? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB:)** Mheshimiwa Spika, kwa kweli tunajua *legal tender* ya fedha ya Tanzania ni shilingi siyo dola. Kwa kweli wanaofanya hivyo ni makosa, kwa sababu malipo yote lazima yawe

kwa shilingi na lazima wafuate hivyo. Serikali hilo italiangalia na itahakikisha kwamba *legal tender* yetu inafuatwa kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa kanuni za Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, la pili kwamba bajeti ni ngumu. Sasa kwa muda wa miaka isiyopungua nane Serikali haijaja na *mini budget* hapa hivyo, ina maana Serikali inapofanya bajeti yake inafanya kwa kuzingatia hayo yote. Kwa hiyo, kama nilivyosema jambo la msingi ni kuhakikisha kwamba ile *foreign currency* inayokuja pia kwa msaada wa *budget support* zingine zinazidisha vilevile uimarishaji wa shilingi. Shilingi hivi sasa ukiangalia inapoteza thamani yake kwa asilimia 5 kwa kila baada ya miaka mitano. Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, yeye ni *banker* analijua hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi ni mwaka 2004 ambapo shilingi hasa ndipo ilipokuwa imeteremka sana. Thamani ya shilingi kwa dola moja ilikuwa shs 1,885.53, lakini kadri hali ilivyozidi kuboreka mpaka mwezi wa Mei, 2006 dola moja ni sawa na shilingi 1262.25. Kwa hiyo, kama nilivyosema shilingi inapanda na wakati mwingine inashuka, lakini hatujafikia kiwango ambacho kinaweza kuharibu bajeti yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge , nilivuta vuta muda lakini sasa nadhani inatosha. Swali hilo moja lililosalia tutalipanga siku ya Jumatatu au siku ya Jumanne. *(Makofi)*

Matangazo, nianze na wageni, kwanza, kwa heshima na taadhima naomba kuwatambulisha Chama cha Wazee Tanzania, Chama chao kinaitwa SAWATA - Saidia Wazee Tanzania. Hawa ni wazee wetu ambao wamekuja kufanya mkutano hapa Dodoma na pia kukutana na Waheshimiwa Wabunge. Wanaongozwa na Mwenyekiti wao Brigedia Jenerali Felix Mbena, naomba asimame pale alipo, yule pale. Brigedia Jenerali Mbena, siyo mgeni kwa wengi wetu hapa, ni mmoja wa Watanzania waliojichomoza katika kulitumikia Taifa letu vyema sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni faraja kubwa kwamba mtu mwenye sifa nzuri sana kama huyu ndiye anayeongoza kama Mwenyekiti wa SAWATA. Nadhani inatupa matumaini kwamba tunakwenda vizuri. Pamoja naye yupo na mwenyeji wake Mzee wetu Harun Sembuche aliyepata kuwa Katibu Mkuu wa Wizara kadhaa katika siku za nyuma, yeye ndiye Mwenyekiti wa SAWATA, Mkoani Dodoma. Pia nimtambulishe Ndugu Sebastian Bulegi ambaye ni Katibu wa SAWATA, Tanzania, yule pale.

Sasa ningewaomba wazee wangu kwa heshima na taadhima msimame Waheshimiwa Wabunge waweze kuwaona tafadhalini, wako 32 pale. Sijui Katiba yao ikoje wengine sioni kama ni wazee sijui wamewasindikiza hawa wazee au vipi! Ahsante sana. Tunawapongeza na kuwashukuru sana. Tutaendelea kupanga fursa muweze kuongea na Waheshimiwa Wabunge. Ahsanteni. Mnaweza kukaa. *(Makofi/Kicheko)*

Kundi la pili, la wageni wetu kwa leo ninafurahia sana kuwakaribisha kwenye *gallery* makada wa Chama cha Mapinduzi waliokuwa wanahudhuria mafunzo. Mnajua

Waheshimiwa Wabunge popote duniani dalili ya chama makini ni kwamba kina mpango wa mafunzo kwa makada wake. Sasa vyama visivyokuwa na sera sawasawa havina cha kufundisha. Lakini Chama cha Mapinduzi kina sera safi, msingi mzuri. Kwa hiyo, nyakati hadi nyakati kunakuwa na mafunzo kwa ajili ya makada. Jambo hili naomba vyama vile vingine siwezi kuvitaja vijaribu kuiga jambo zuri hili katika kujiimarisha. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, makada wa CCM waliomaliza mafunzo ya wiki kadhaa siyo semina ya siku mbili ni mafunzo kabisa. Hawa wanatoka Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Mbeya, Iringa na Ruvuma. Jumla yao wako kiasi cha 80. Miongoni mwao napenda kuwataja wachache tu kwa mfano, Ndugu Mujuni Kataraiya, aliyekuwa Mbunge mwenzetu katika kipindi kilichopita na sasa ni Katibu wa CCM Mkoa wa Singida. Yupo pia Ndugu Chizi, Katibu wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam na ni kiboko sana kwa kampeni huyo. *(Makofi)*

Sasa niseme tu kwamba kwa kuwaenzi wenzetu, hawa ni sehemu ya ile *engine* iliyosaidia ushindi. Waheshimiwa ndugu zetu makada hapa kwa juhudi zenu mliwezesha Waheshimwia Wabunge wa CCM kuwa 274 na tukawaachia wenzetu viti 45. Tunawaomba mwaka 2010 mpandishe kidogo hiyo idadi. *(Makofi)*

Karibuni sana, nawaomba sasa msimame ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwatambua na kuwaenzi. Ahsanteni sana. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, ningeomba nyote muweze kukaa ila abaki amesimama Mheshimiwa Othman Ndunga aliyehama kutoka *CUF* juzi na sasa ni Katibu wa CCM Wilaya. Huyu ni Katibu wa CCM wa Wilaya mpya ya Kilolo. Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge baada ya utambulisho kabambe huo. *(Makofi)*

Sasa niendelee, kuna mgeni wa Mheshimiwa Juma Akukweti, anatoka kule Tunduru ni Ndugu Zubeir Hazidu ambaye alikuwa meneja wa kampeni ya Mheshimiwa Juma Akukweti, yule pale. Karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale ameniomba nitangaze wageni wake ambao ni Mganga Mkuu wa Wilaya ya Liwale Dr. Maokola, yule pale mkono wa kulia, Afisa Elimu wa Elimu ya Liwale, Mama Maochela yule pale na Mhandisi wa Wilaya ya Liwale, Ndugu Buhoma. Karibuni sana. Tunafurahi mara kwa mara kuona wageni wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Elizabeth Batenga, ameniomba nitambulishe kijana wake Josephat Marko Ngajilo, ambaye amemaliza kidato cha sita katika Sekondari ya Dakawa, Morogoro mwaka jana, yule pale. Karibu sana kijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, ameniomba nitambulishe wageni wake wa kwanza, ni Ndugu Glasiasi Kipara, Mwenyekiti wa Wachimbaji wadogo wadogo wa madini kule Mbinga, yule pale. Pamoja na Ndugu John Lwabano ni mjumbe katika chama hicho cha wachimbaji wadogo wadogo wa madini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sehemu ya pili ya haya matangazo. Kama baadhi yenu mnavyofahamu Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Ali Haroon Suleiman ambaye pia ndiye Waziri wa Elimu kule Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, alifiwa na mama yake mzazi tarehe 13 Septemba, 2006. Msiba huo kama nilivyotangaza ni kwamba umetokea katika kipindi ambacho Bunge halikuwa linakutana. Kwa hiyo, kwa mujibu wa utaratibu tuliojiwekea Ofisi ya Bunge itaandaa bahasha ili tuweze kumshika mkono mwenzetu, ndiyo utamaduni wetu na ndiyo utaratibu wetu.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu matangazo ya Kamati, Waheshimiwa Wabunge wote ambao walikwenda ziara ya mafunzo nchini Singapore, wanaombwa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Omar Kwaangw' kukutana leo saa 5.00 asubuhi chumba namba 219. Waliokwenda Singapore ziara ya mafunzo watakuwa na mkutano leo saa 5.00 chumba namba 219. *(Makofi)*

Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* Mwenyekiti wake Mheshimiwa John Cheyo, anawaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo saa 5.00 asubuhi chumba namba 428. Kamati ya Hesabu za Serikali saa 5.00 asubuhi hii wakutane katika chumba namba 428 jengo la utawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi anawaomba wajumbe wakutane saa 10.00 jioni leo, ghorofa ya pili, jengo la utawala. Kamati ya Fedha na Uchumi wakutane saa 10.00 jioni kwa kikao kifupi sana anavyosema Mwenyekiti, pale ghorofa ya pili.

Taarifa ya Semina, kesho Jumamosi itakuwepo Semina kwa Waheshimiwa Wabunge wote iliyoandaliwa na Wizara ya Fedha. Semina hiyo inahusu Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu (*Anti-Money Laundering)* itafanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa tatu asubuhi. Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria semina hiyo muhimu. *(Makofi)*

Pia siku ya Jumapili, tutakuwa nayo semina nyingine ambayo ni ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, inahusu Mahusiano katika *Great Lakes Regions* itaanza saa 5.00 asubuhi ni ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Waheshimiwa Wabunge, nawaomba Wajumbe wote wa Tume ya Huduma za Bunge tukutane saa 7.30 mchana Ofisini kwangu mchana huu. Pia Kamati ya Uongozi itakuwa na kikao kifupi kesho saa tatu asubuhi katika ukumbi wa Spika kabla ya semina. Saa tatu asubuhi kikao kifupi.

Naomba nitoe taarifa zifuatazo kuhusu Kamati mbalimbali. Waheshimiwa Wabunge. Mtakumbuka niliituma Kamati ya Ulinzi na Usalama ichunguze madai ya Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mbunge wa Tarime kuhusu mauaji kule Tarime ambayo yeye alidai yalisukumwa kisiasa. Hadi sasa sijapata taarifa kwa hiyo, mwelekeo unaonekana kwamba sitaweza kutoa taarifa kwenu kwa Mkutano huu wa Tano. Kwa hiyo, naona suala hili litasogea hadi Mkutano wa Sita.

Kwa taarifa yenu tu ni kwamba tunao uwezekano mkubwa kwamba shughuli zote za Bunge zitakuwa zimekwisha siku ya Jumatano asubuhi wiki ijayo. Sijaipata taarifa kwa hiyo sina cha kutoa taarifa. *(Makofi)*

Kamati nyingine niliyoituma kazi ni Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Ilihusu maneno waliyotupiana Mheshimiwa Adam Malima, Mbunge wa Mkuranga na *IPP Media.* Kwa bahati mbaya nayo hadi sasa ninavyozungumza hapa sijapewa taarifa ya kuweza kuwasilisha kwenu. Kwa hiyo, hiyo nayo naisogeza iende kwenye Mkutano wa Sita mwezi Januari, 2007.

Kamati ya Kilimo na Ardhi, niliikabidhi tuhuma ambazo zilitolewa na Mheshimwia John Cheyo, dhidi ya Mheshimiwa John Shibuda na Bodi ya Elimu ya Sekondari kule Shinyanga. Hii Kamati imekamilisha kazi yake na imenikabidhi. Sasa hivi inafanyiwa uchambuzi na wataalam wa kisheria. Sasa ili mambo yapendeze nadhani zote pamoja na hii iliyokuwa tayari niziwasilishe pamoja katika Mkutano Sita. *(Makofi)*

Naomba kutoa taarifa kwamba suala la ukarabati wa Kanuni za Bunge tunaendelea nalo. Sasa hivi kilichojitokeza ni kwamba kwa kuwa marekebisho yaliyopendekezwa na Tume ya Mheshimiwa Job Ndugai, ni mapana na ya kina yanahusu masuala mengine ambayo yanagusa Katiba, mengine yanagusa Sheria na yapo yale ya kawaida.

Kwa hiyo, wataalam wa Sheria katika Ofisi ya Bunge hivi sasa wanafanya uchambuzi kwa misingi hiyo. Kwa hiyo, haitawezekana kuwa na taarifa yoyote ya kuwasilishwa na wala Kamati ya Kanuni haiwezi kuitwa kuzingatia kwa sababu kazi hiyo bado inaendelea. Ni kazi nzuri lakini ni kubwa ina mambo mengi ambayo yanahitaji kutafakari na kushirikisha vyombo mbalimbali.

Kwa hiyo, kwa kiasi kile yale ambayo yatastahili kubadili Kanuni zetu. Kwa mfano, uhariri tu wa kupanga vizuri ili Waheshimiwa Wabunge msiwe na shida katika kufanya rejea katika Kanuni, hayo nadhani tunaweza kuyazingatia katika Mkutano wa Sita mwezi Januari, 2007.

Waheshimiwa Wabunge, lakini yale ambayo yanagusa Katiba na Sheria nyingine nzito nzito hivi ni dhahiri kwamba yana utaratibu wake na itabidi ule ufuatwe kwa yale ambayo yatakubalika. Vinginevyo mengine yataahirishwa tu kwa sababu si ya lazima. Ieleweke tu kwamba mapendekezo ya awali ya Tume ya Mheshimiwa Job Ndugai si kwamba yote yalikuwa yamekubaliwa na Ofisi ya Bunge. Kwa hiyo, utaratibu utaendelea, tutaanza na yale ambayo ni mepesi kwa Mkutano wa Sita, Januari, 2007. Halafu mengine yatachukua nafasi yake katika uhai wa Bunge hili. *(Makofi)*

Mwisho, nilikuwa nimempa hadi leo Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, ili aniombe radhi kwa matamshi yake ya kifedhuli kabisa nje ya Bunge hili. Kumtuhumu Spika kutokujua Kanuni ni utundu sijui, ni utoto sijui, maana

yake ukishaharibu kiti maana yake unavunja imani ya aliyekalia kiti hiki kuendesha Shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ndiyo maana Kanuni zetu zimeweka utaratibu wa kumkosoa Spika ndani ya Bunge. Huyo mwenzetu hakufuata hilo. Lakini mbaya zaidi sasa inasemekana nimepata taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Halima Mdee, nadhani wanafanya kazi kwa karibu sana hawa.

Mheshimiwa Halima Mdee, aliniambia jana kwamba Mheshimiwa Kabwe Zitto, ameenda Ujerumani. Ameenda Ujerumani bila hata kutoa taarifa kwa Spika, hili ni kosa lingine tena. *(Makofi)*

Mimi nadhani kwa sababu nasubiri, hili lazima nitalipeleka kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Mbunge kuondoka wakati wa Mkutano wa Bunge, anaondoka tena anakwenda nje ya nchi bila kutoa taarifa yoyote kwa Spika ni kosa, nitalipeleka huko. Lakini nasubiri sasa kama yuko tayari kuomba radhi kwa lile la kwanza. Kama hayuko tayari kuomba radhi na anajiona anajua, basi hilo nalo sasa litachanganywa na hili yote mawili yatapelekwa kwenye Kamati yetu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili waweze kunishauri hatua za kuchukua. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, nawashukuru sana kwa uvumilivu wenu. Nakwenda sasa kujiandaa kwa Mkutano wa Tume ya Huduma za Bunge. Ningemwomba Mwenyekiti Mheshimiwa Job Ndugai, aje hapa akalie kiti. *(Makofi)*

*(Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia kiti)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Kabla sijamwita Katibu, nimtambulishe Katibu wa CCM Wilaya ya Kongwa, Mama Daima Mbwayo. *(Makofi/Kicheko)*

**AZIMIO**

**Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Ushirikiano Kati ya nchi za Jumuiya ya Ulaya na Umoja wa Nchi za Afrika, Pacific na Caribbean *(The Cotonou Partnership Agreement)***

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Ushirikiano Kati ya nchi za Jumuiya ya Ulaya na Umoja wa Nchi za Afrika, Pacific na Caribbean ujulikanao kama *The Cotonou Partnership Agreement.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili lilijadiliwa na kupata ridhaa ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi katika kikao chake kilichofanyika tarehe 27 Oktoba, 2006 Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya Uenyekiti wa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima, Mbunge wa Mkuranga pamoja na Wajumbe wote na Kamati hiyo kwa maoni yao mazuri yenye lengo la kuboresha Azimio hili. Aidha, napenda pia kushukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano walioonyesha wakati wa kuwasilisha Azimio hili mbele ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazofadhiliwa na Jumuiya ya nchi za Ulaya kupitia Mkataba ujulikanao kama *The Cotonou Partnership Agreement* ambao ulisainiwa mnamo tarehe 23 Juni, 2000 mjini Cotonou nchini Benin baina ya wawakilishi wa nchi 77 za Umoja wa nchi za Afrika, Caribbean na Pacific ikiwemo Tanzania na nchi 25 za Jumuiya ya Ulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali Mkataba huu uliridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Azimio Namba 4 la tarehe 10 Agosti, 2001 ambapo utekelezaji wake ni kwa kipindi cha miaka ishirini (2000 – 2020) katika awamu nne za miaka mitano, mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya mkataba huu ni kuzisaidia nchi wanachama za Afrika, Carribean na Pacific kujenga uchumi endelevu ili kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa umaskini. Katika kufanikisha shabaha hii maeneo manne makubwa ya ushirikiano yanayonufaika na mkataba huu ni siasa, utamaduni, uchumi na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida inayopata Tanzania kutokana na Mkataba wa Cotonou, Tanzania kama mwanachama wa umoja huu, inafaidika kwa mikopo ya masharti nafuu inayotolewa na Benki ya Rasilimali ya nchi za Ulaya. Aidha, katika kipindi cha kwanza cha miaka mitano (2000 - 2005), Tanzania imenufaika kwa kiasi kikubwa kupitia misaada inayotolewa na miradi inayofadhiliwa na nchi za Ulaya kwa utaratibu wa Bahasha "A" na Bahasha "B" kama ifuatavyo:-

Bahasha A, Mradi wa kuchangia katika Bajeti ya Taifa *(Budget Support Programme)* kwa ajili ya kugharamia sekta za huduma za jamii, Mradi wa kufadhili Mpango wa Sekta ya Elimu, miradi ya miundombinu kama vile ujenzi wa bandari ya Zanzibar, barabara za Isaka-Tinde-Nzega, Morogoro hadi Dodoma, barabara za Jiji la Mwanza.

Aidha, kiasi cha *Euro* milioni 3.8 zilitolewa kusaidia Asasi Zisizo za Kiserikali, mchango kwa ushirikiano wa kibiashara katika nchi zilizomo Kusini mwa Afrika *(SADC)* na Umoja wa Ushirikiano wa Nchi za Afrika Mashariki na mchango katika maendeleo ya sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bahasha "B," chini ya utaratibu huu kiasi cha *Euro* milioni 6.5 zilitolewa kuchangia mfuko wa kulinda amani katika nchi za Afrika ambapo Tanzania ni mwanachama. Aidha, kiasi cha *Euro* milioni 59.7 kilihamishwa kutoka Bahasha "B" kwenda Bahasha "A" ili kuongeza fedha za utekelezaji katika maeneo yaliyoainishwa chini ya utaratibu wa Bahasha "A."

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya *STABEX*, chini ya programu hii kiasi cha *Euro* milioni 44 kilitolewa kwa ajili ya mfuko wa *STABEX* kugharamia mambo yafuatayo:-

(i) Utafiti wa zao la Kahawa *(Euro* milioni 13.5);

(ii) Sekta ya Kilimo *(ASDP) Euro* milioni 18;

(iii) Ujenzi na ukarabati wa barabara za vijijini kwa mikoa inayolima zao la kahawa *(Euro* milioni 12); na

(iv) Uratibu na Ufuatiliaji *(Euro 0.9).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya barabara zenye urefu wa kilometa 635.3 zinajengwa na kukarabatiwa kupitia fedha hizi katika mikoa inayolima zao la kahawa ya Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Ruvuma, Kagera, Mara, Kigoma na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kuainisha barabara zilizopangwa kukarabatiwa na kujengwa kwa fedha za *STABEX* ilifanywa na Wizara ya Kilimo na Chakula. Serikali iliteua Wakala wa Barabara Nchini *(TANROADS)* kutafuta

wakandarasi wa barabara na kusimamia Wakandarasi hao katika ujenzi na ukarabati huo.

Mheshimiwa Spika, aidha, fedha kwa ajili ya malipo kwa Wakandarasi wa miradi hii ya barabara zinatolewa na Wizara ya Fedha kupitia *TANROADS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa mazungumzo yanaendelea kati ya Serikali na Jumuiya ya nchi za Ulaya kuhusu maeneo ambayo yatafadhiliwa na mpango wa Mfuko wa maendeleo wa kumi *(EDF 10)* wa Jumuiya ya nchi za Ulaya ambayo imetenga kiasi cha awali cha cha *Euro 550* milioni kwa Tanzania kwa ajili ya hiyo. Maeneo ambayo yana mwelekeo wa kufadhiliwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Uchangiaji katika Bajeti ya Taifa kwa ajili ya kupunguza umaskini *(Poverty Reduction Budget Support Programme)* asilimia 75 katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kuchangia Bajeti ya Serikali;

(b) Miradi ya Miundombinu; na

(c) Elimu.

(ii) Biashara na mahusiano ya kikanda *(Trade and Regional Integration)* asilimia 14 katika maeneo yafuatayo:-

(a) Biashara;

(b) Kilimo na Uvuvi; na

(c) Mawasiliano na Uchukuzi.

(iii) Utawala na Uwajibikaji *(Governance and Accountability)* asilimia 11 katika maeneo yafuatayo:-

(a) Utawala bora;

(b) Kusaidia Asasi Zisizo za Serikali; na

(c) Mchango wa kuendesha ofisi ya Mlipaji Mkuu wa *EDF (Support to the office of the National Authorising Officer for EDF).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 25 Juni, 2005 nchi wanachama wa Umoja wa nchi za Afrika, Carribbean na Pacific na zile za Jumuiya ya Ulaya kupitia mkutano uliofanyika nchini Luxembourg, zilifanya marekebisho mbalimbali katika Mkataba wa *Cotonou Partnership Agreement* wa mwaka 2000 yenye lengo la kuboresha

utekelezaji wa mkataba huu ikiwa ni pamoja na kuweka utaratibu mpya wa kuendesha miradi inayofadhiliwa na nchi za Umoja wa Ulaya kwa nchi wanachama wa *ACP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia marekebisho haya, nchi wanachama wa *ACP* wanapaswa kuridhia marekebisho haya kabla ya tarehe 31 Desemba, 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa niwasilishe maelezo ya marekebisho yaliyofanyika kama ifuatavyo:-

(i) Kipindi cha utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa chini ya Mkataba wa Cotonou kimeongezwa kutoka miaka mitano hadi sita kuanzia Januari 1, 2008 yaani (2008 - 2013), badala ya miaka mitano tu ya sasa.

(ii) Kutoa upendeleo wa mikopo au misaada kwa nchi wanachama wa *ACP* zilizoathirika na majanga ya asili, vita, na zilizo katika mpango wa kusamehewa madeni wa *HIPC* au mpango wowote wa kimataifa unaohusu udhibiti endelevu wa madeni.

Aidha, nchi wanachama zenye mahitaji maalum au zitakazoonyesha ufanisi mkubwa katika matumizi ya misaada inayotolewa zinaweza kuongezewa fedha.

(iii) Kuboresha utaratibu wa maombi ya fedha *(Financing Proposals)* ambapo sasa maombi yataidhinishwa ndani ya nchi husika badala ya utaratibu wa zamani wa kuwasilisha maombi *EU Commission* kwanza. Aidha muda wa kutoa maamuzi ya maombi ya kifedha umepunguzwa kutoka siku 120 mpaka siku 90. *(Makofi)*

(iv) Kuhusu zabuni zitakazotolewa na kufadhiliwa na nchi wanachama wa Umoja wa Jumuiya ya Nchi za Ulaya, upendeleo maalum utatolewa kwanza kwa Makampuni ya nchi wanachama wa *ACP*, pili kwa mzabuni atayeshirikiana na makampuni ya nchi wanachama wa *ACP* na tatu, mzabuni atakayeruhusu matumizi ya vifaa na nguvu kazi kutoka nchi mwanachama wa *ACP*.

(v) Kutoa misaada kwa nchi wanachama ambazo zitaathirika na kushuka kwa mapato ya uuzaji wa bidhaa nje na hivyo kusababisha kushuka kwa uchumi na kuathirika kwa sera za kiuchumi za nchi hiyo.

(vi) Kuzielekeza nchi wanachama kushirikiana katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kupambana na magojwa yatokanayo na umaskini kama vile malaria, kifua kikuu na afya ya uzazi na kulinda haki za wanawake.

(b) Kusaidia Taasisi za kijamii ziweze kutoa huduma za kijamii kwa watoto wasio na uwezo na walioathirika kisaikolojia kutokana na migogoro ya vita.

(c) Kusaidia miradi au shughuli za kiuchumi zitakazotekelezwa baina ya nchi wanachama na nchi zisizo wanachama wa Umoja huu.

(vii) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la ushirikiano katika masuala ya kifedha yamefanyika marekebisho ili kuziwezesha Taasisi zilizosajiliwa katika nchi zisizo wanachama na zilizokubaliwa na nchi wanachama wa *ACP*, Mabunge ya nchi wanachama na Nchi zinazoendelea ambazo sio wanachama wa *ACP* zenye umoja wa kikanda kama vile Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, *SADC* pamoja na nchi wanachama wa *ACP* kupata misaada ya kifedha kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Ulaya. *(Makofi)*

(viii) Kwa upande wa ushirikiano katika masuala ya kisiasa yamefanyika marekebisho ili kuwezesha nchi wanachama:-

(a) Kupambana na kuzuia mamluki wa kivita;

(b) Kuridhia na kutekeleza mkataba wa *Rome Statute of International Criminal Court;*

(c) Kushirikiana katika kupambana na ugaidi kwa kupeana taarifa kuhusu vikundi vya kigaidi na mitandao yao, kubadilishana ujuzi/mafunzo ya kupambana na ugaidi na kuzuia matumizi ya silaha za maangamizi.

(ix) Kuwezesha Taasisi na Asasi zisizo za Kiserikali kupata misaada ya kifedha moja kwa moja kutoka *EU Commission* bila kupitia kwa Serikali ya nchi husika. *EU Commission* itatoa taarifa kwa *National Authorising Officer* wa Serikali ya nchi husika kuhusu misaada au miradi inayogharamiwa kupitia kwa Asasi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya marekebisho mengine ni ya kiujumla yenye kutoa ufafanuzi au kufanyia marekebisho vifungu vya Mkataba ili kuwezesha vifungu hivyo visomeke vizuri na kueleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la kuridhia marekebisho ya Mkataba wa Ushirikiano Kati ya nchi za Jumuiya ya Ulaya na Umoja wa Nchi za Afrika, Pacific na Caribbean yaani *The Cotonou Partnership Agreement* kama ifuatavyo:-

KWA KUWA kwa mara ya kwanza Tanzania iliingia Mkataba wa *Cotonou Partnership Agreement* mwaka 2000 utakaodumu kwa kipindi cha miaka 20, yaani 2000 - 2020;

NA KWA KUWA Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazonufaika na Jumuiya ya nchi za Ulaya chini ya Mkataba wa Cotonou;

NA KWA KUWA Mkataba huu uliridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Azimio Namba 4 la mwaka 2001;

NA KWA KUWA Mkataba huu ulifanyiwa marekebisho na kusainiwa na wawakilishi wa nchi zote 77 wanachama wa *Africa, Caribean* na *Pacific (ACP)* ikiwepo

Tanzania na nchi 25 za Jumuiya ya nchi za Ulaya mnamo mwezi Juni 2005, ambapo kwa mujibu wa masharti ya mkataba huu, marekebisho haya yatakubalika na kuanza kufanya kazi baada ya theluthi mbili ya nchi za *ACP* na nchi za Ulaya kuridhia;

NA KWA KUWA marekebisho ya Mkataba huu yataendelea kufungua masoko ya Jumuiya ya nchi za Ulaya kwa ajili ya bidhaa kutoka Afrika, na pia yataharakisha matumizi ya fedha zilizotengwa kwa Tanzania;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na marekebisho ya Mkataba huu kwa Tanzania na kwa wanachama wa nchi za *Africa*, *Caribbean* na *Pacific* na nchi nyingine zinazoendelea, na pia umuhimu wa kukubali kufanya marekebisho ya Mkataba huu, Bunge hili katika Mkutano wa Tano na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, linaazimia kwamba:-

(a) Marekebisho ya Mkataba uitwao *Cotonou Partnership Agreement* kati ya nchi wanachama za Afrika, *Caribbean* na *Pacific* na Jumuiya ya Nchi za Ulaya yaridhiwe ili Tanzania iweze kunufaika na hivyo kujenga uchumi endelevu ili kupunguza na hatimaye kuondoa umasikini; na

(b) Wizara ya Fedha iendelee kusisimamia kwa karibu zaidi sekta zote pamoja na AZISE/ASASI ambazo zinapata misaada na mikopo kupitia utaratibu huu ili Taifa liweze kunufaika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo zaidi kuhusu marekebisho haya yapo kwenye makabrasha ambayo naamini Waheshimiwa Wabunge wamepata nakala yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru. *(Makofi)*

Kabla sijamwita Msemaji wa Kamati ya Fedha na Uchumi, nitoe tangazo moja tu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa safari nje ya Dodoma. Kwa hiyo, Shughuli za Serikali Bungeni, zitakaimiwa na Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib. *(Makofi)*

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 63(3)(e) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Bunge litajadili na kuridhia Mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano, ambayo kwa masharti yake inapaswa kuridhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni ya 88(9) ya mwaka 2004. Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ilipata fursa ya kuupitia Mkataba uliowasilishwa na Mheshimiwa Zakia H. Meghji, Waziri wa Fedha mbele ya Kamati hii ili kujadiliwa na kupata maoni na ushauri wa kuliwezesha Bunge lako tukufu kujadili na kuridhia marekebisho ya Mkataba huu ujulikanao kama Mkataba wa Ushirikiano Kati ya

nchi za Jumuiya ya Ulaya na nchi za Umoja wa Afrika, Caribbean na Pacific *(Cotonou Partnership Agreement). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kuhusu Azimio la kuridhia marekebisho ya Mkataba wa Kimataifa uliowasilishwa na Serikali kama ulivyotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi zake za kuendeleza na kukuza mahusiano ya kisiasa, utamaduni, uchumi na biashara kati ya Tanzania na nchi za Jumuiya ya Ulaya na nchi za Umoja wa Afrika, Caribbean na Pacific.

Mheshimiwa mwenyekiti, ni dhahiri kabisa uhusiano huu unaifaidisha na kuinufaisha Tanzania kwa mikopo ya masharti nafuu inayotolewa na Benki ya Rasilimali ya nchi za Ulaya na misaada inayotolewa na nchi za Ulaya kwa ajili ya kuboresha sekta za elimu, miundombinu, *NGOs,* utalii, biashara, bajeti, kilimo na kadhalika. Kamati inashauri Serikali mahusiano haya yawe endelevu kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa mwenyekiti, kutokana na marekebisho yaliyofanyika, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia na kusimamia vyema matumizi ya fedha zinazopatikana kutokana na Mkataba huu ili tupate *value for money* na hatimae tuweze kupata fursa zaidi za kuboresha uchumi wa nchi yetu na hatimae kupunguza umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa Mkataba huu ambao unalenga kuboresha sekta za elimu, kilimo, biashara, miundombinu na kadhalika. Kamati inashauri Serikali iweke mikakati bora zaidi ya kuwezesha utekelezaji wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali iweke njia nzuri za kusimamia na kukagua maendeleo na ubora wa miradi itokanayo na Mkataba huu. Aidha, kuwe na usimamizi mzuri wa mchakato wa kutoa zabuni za ujenzi wa barabara zetu ili kuepukana na baadhi ya matatizo yanayojitokeza sasa hasa ya ucheleweshaji wa kukamilisha barabara hizo kwa kipindi kilichopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeeleza faida zitokanazo na Mkataba huu lakini haijaeleza matatizo yatokanayo na masharti ya utekelezaji wa Mkataba huu. Kamati inashauri kuwa, Serikali ieleze pia matatizo yatokanayo na utekelezaji wa Mkataba huu hususan yatokanayo na urasimu usio wa lazima pamoja na tatizo la kuelekeza rasilimali hizi maeneo ambayo hayazingatii ukuaji wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kumshukuru Mheshimiwa Zakia H. Meghji, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Naibu Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Mustafa H. Mkullo, Naibu Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wote wa Wizara yake kwa kuwasilisha Azimio hili kwa ufasaha jambo ambalo limerahisisha kazi kwa Kamati yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwneyekiti, kwa ujumla marekebisho yote yaliyofanywa yameashiria utaratibu mzuri wa kutumia rasilimali zitokanazo na Mkataba huu kwa nchi yetu, tukizingatia uimara wa ufuatiliaji, usimamizi na utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa kazi yao nzuri walioifanya ya kupitia na kuchambua Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ya Fedha na Uchumi imejadili na kuchambua Azimio na imeridhika nalo. Kwa hiyo basi Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu kujadili na hatimae kuridhia Azimio na marekebisho ya Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Mkaofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, tunakushuru sana! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, niseme tu kwamba nina maombi mawili mpaka sasa ya wachangiaji, Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi na Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, wajiandae. Kama kuna Waheshimiwa wengine ambao wangependa kuchangia, basi fursa ipo! *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (k.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Upinzani ambaye pia ndiye Kiongozi wetu wa Upinzania hapa Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya hii kuhusu Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Ushirikiano kati ya nchi za Jumuiya ya Ulaya na nchi za Umoja wa Afrika, Carribean na Pasific *(Cotonou Partinership Agreement). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata wasaa huu wa kutoa maoni ya kambi yetu kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(c) na 70(2) toleo la mwaka 2004, kuhusu kuridhia mkataba uliotajwa hapo juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kuwa Mkataba huu wa ushirikiano ulisainiwa mwaka 2000 na Bunge lako Tukufu likauridhia mwaka 2001 mwezi wa nane, japokuwa utekelezaji ni wa miaka 20, lakini nchi mwanachama zinatakiwa kila baada ya miaka mitano na kama tulivyoelezwa sasa hivi hapa imeongezwa kuwa sita, kuridhia upya mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kuwa kundi la *ACP* ndilo lilikuwa la kwanza kuanzishwa hapo 6 Juni, 1975. Kundi hili liliungana na Kundi la *EU* mwaka 2000. Kwa kipindi chote hicho cha kuwepo kwake kiuchumi na kibiashara Tanzania kama nchi mwanachama imenufaika vipi? Au ni ukweli kuwa bado inabebwa na Kundi la *EU?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuridhia kwa awamu ya miaka mitano mitano ni kutoa nafasi na kama tulivyoelezwa sasa hivi ni sita kuanzia mwezi wa nane mwaka unaofuta, kwa nchi mwanachama kutoa tathmini ya faida ama hasara ya kuwamo katika ushirikiano huo. Kwa hiyo na sisi Tanzania naamini hatuna sababu yoyote ile ya kutokuridhia kwa kuangalia faida ambazo tumezipata katika nyanja mbali mbali za kiuchumi, biashara, siasa na utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ijapokuwa katika mkataba inaonyesha kuwa nchi mwanachama zitanufaika sana na misaada kutoka jumuiya ya nchi za ulaya kitu ambacho ni kweli, lakini kitu cha kuangalia ni je, ushirikiano huu unatusaidia sisi kama nchi kukuza uwezo wetu kwa kupata masoko ya bidhaa zetu katika nchi za Ulaya? Kama ambavyo wao wanauza bidhaa zao katika nchi zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Economic Partnership Agreement (EPA) at Regional Economic Community (REC)* inaonyesha kuwa Umoja wa Jumuiya ya nchi za Ulaya inafaidika zaidi kwa kujipanua zaidi kimasoko kwa kulinganisha na mataifa yaliyomo katika jumuiya mbali mbali kama vile, *ESA*, *ECOWAS*, *CEMAC*, *EAC*, *COMESA* au *SADC* na kadhalika. Kwa maana hiyo mfumo wa faida kibiashara hauko *direct proportional but inversely proportional*.

Kwa ufanyaji wa biashara wa aina hii ni ukweli kwamba unaathiri ukuaji wa jumuiya zetu za Ushirikiano wa kiuchumi katika bara letu la Afrika, kwani nchi za ulaya ndizo zitakazokuwa zinanufaika zaidi na masoko ya bidhaa zao kutokana na ukweli kuwa bado hatujaweza kushindana nazo katika kutoa ubora wa bidhaa za viwandani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya makubaliano ya *ACP-EU* ni kusaidia ku-*diversify* kile kinachozalishwa na nchi mwanachama. Wakati ule ule nchi mwanachama katika *EPA* zinasisitiza jinsi ya kupunguza ushuru kwa bidhaa zinazozalishwa na kuingizwa baina ya nchi mwanachama. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani inaamini kuwa, hakuna nchi ambayo itapata maendeleo ya viwanda bila ya kuwa na sera ya kutoza ushuru kulingana na aina na faida ya biashara kwa nchi. Ushuru ndiyo njia pekee ya kulinda bidhaa za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi ushirikiano na maudhui ya ushirikiano wa *ACP-EU* ndani ya *EPA* ni njia au ujanja wa maksudi ili tuendelee kwa wachuuzi wa bidhaa kutoka nchi nyingine kwani hatutakuwa na uwezo wetu binafsi wa kujenga viwanda kwa ajili ya kuzalisha bidhaa zetu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana hii inapata baraka kuwa hata mikopo inayotolewa inakuwa tayari imekwishaonyesha ni kwa ajili ya kitu gani na kubadilisha matumizi ya mkopo huo ni kosa. Je, kwa njia hii tunaweza kuwa na uhuru wa kupanga miradi yetu kulingana na vipaumbele vyetu au tunakwenda na kulingana na wahisani wanataka nini ingawa siyo moja kwa moja!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli uliowazi kuwa nchi za Jumuiya ya Ulaya haziwezi kuruhusu ushindani wa aina yeyote ya kibiashara toka nchi mwanachama wa *ACP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dhana nzima ya ushirikiano wa kikanda katika nchi za Afrika ni kupunguza nguvu za mataifa ya Ulaya katika kushikilia biashara ya mataifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa dhana nzima ya ushirikiano huu kwa njia moja ama nyingine nchi za kiafrika zinajikuta zimeishajifunga mnyororo wa ukoloni mamboleo ambao haziwezi kuuvua kabisa na ile dhana ya uanzishwaji wa ushirikiano wa kikanda baina ya nchi zetu katika bara letu inapoteza mwelekeo na mwisho huenda ushirikiano huu ukafa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, tunaamini kabisa katika ushirikiano wa aina yoyote ile ambapo washiriki wanakuwa hawako katika mazingira yanayolingana basi ni dhahiri faida haziwezi kuwa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,na hili linadhihirishwa na wasiwasi tuliokuwa nao sisi Watanzania juu ya uundwaji wa shirikisho la Afrika ya Mashariki ambapo mpaka sasa tunaamini kuwa wenzetu wa Kenya na Uganda wako mbele zaidi kutuzidi, hivyo wao watanufaika zaidi kuliko sisi, jambo ambalo ni ukweli kwa zaidi ya 70%. *(Makofi)*

Hivyo na dhana hiyo hiyo bado ipo katika ushirikiano wa *ACP EU*. Tukumbuke kwamba hakuna mtu anayeweza kutoa msaada wa mabilioni bure eti ili na wewe uweze kupata nguvu za kuweza kushindana naye. Ni lazima kuna faida fulani ambayo japokuwa haiko wazi kwa kila mtu, lazima tuwe waangalifu sana kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi la uanzishwaji wa ushirikiano huu wa *Cotonou* lilikuwa ni kuondoa umaskini, basi sasa je, toka kuridhiwa kwa Mkataba huu yapata miaka mitano: Je, tathimini yetu ikoje baina ya nchi ya wanachama, umaskini umeongezeka au umepungua na ilikuwaje kabla ya *EU* kuingia katika ushirikiano huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, kuhusu fedha za *STABEX* kama ambavyo imeelezwa hapa kuwa ni msaada kutoka *EU* Kambi ya Upinzani, inamwomba Mheshimiwa Waziri atupe tathimini yake kama kweli lengo la msaada huo lilisaidia nchi wanachama au hapana kwani taarifa za hapa kwetu zinaonyesha kuwa *EU* wameamua kuachana na *program* ya *STABEX* kutokana na ukweli kwamba haikuzaa matunda yaliyotegemewa na malalamiko yamekuwa mengi sana kwa matumizi ya fedha hizo katika nchi zilizolengwa, yamekuwa ni mabaya na pengine Tanzania ikiwa mojawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, kwa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani. Sasa tunaingia kwenye mjadala na kama nilivyosema, wachangiaji wetu ni wawili, tutaanza na mwakilishi wetu kwenye Bunge la *ACP EU* Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi na atafuatiwa na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii.

Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha, Manaibu wake, Katibu Mkuu na viongozi wengine wakubwa wa Wizara hii na wale wengine wote wanaoshughulikia Muswada wa *Cotonou,* Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Fedha, Wizara ya Mipango na Wizara mbalimbali ambazo zinashughulikia jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiwango fulani nimemsikiliza Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa akisoma hoja iliyopo mbele yetu juu ya Muswada huu. Naomba niseme hivi, Muswada wa *Cotonou* ulipotoka kwa mara ya kwanza na kusainiwa mwaka 2000 uliwafurahisha wengi katika nchi za *ACP*. Uliwafurahisha kwa sababu ulikuwa unazungumzia mikakati mikubwa ya ku-*address* mipango mizima ya maendeleo ya nchi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *Agreement* yenyewe wanazungumzia kitu kinaitwa, *The Development Dimension* na masuala yote ya *development*, masuala yote ya *trade* yamekuwa *addressed* katika Mkataba mzima. Ukiangalia jinsi yanavyoshughulikiwa Muswada wenyewe ni mzuri sana. Ninyi wenzangu ninawashukuru sana kwa sababu mlinichagua mimi kuwawakilisha katika *ACP EU Join Parliamentary Assembly,* nawashukuru sana. *(Makofi)*

Sasa ni mwaka wangu karibu wa sita nikiwakilisha Bunge hili. Naomba niwaambie pengine baadhi ya *experience* zangu kuhusu Muswada huu. Muswada huu unashughulikiwa kwa mpango wa kitu kinaitwa *(EDF) European Development Fund* fedha za ku-*finance* miradi yote au mipango ya maendeleo ya Muswada huu inatokana na *fund* inayoitwa *The European Development Fund.* Hii *European Development Fund* kila nchi ina Afisa ambaye ndiye anaratibu mpango mzima. Hapa kwetu ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, ndiye anayeratibu mipango yote. Kwa bahati mbaya matakwa ya kutoa fedha chini ya mpango wa *EDF* ni *very bureaucratic*. Tumekuwa tukiomba wabadilishe utaratibu mzima kwa sababu wana *demand capacity* ambayo pengine nchi maskini hawana na wao hawajatusaidia kuendeleza hiyo *capacity* katika nchi yetu.

Lakini kusema kweli nchi zetu zimekuwa zinajitahidi sana kufuata vile wanavyosema. Walivyoona sasa na sisi tunaendelea vizuri sasa wamebadilisha utaratibu, wame- *annualize* mpango mzima wa kutoa fedha zamani kama chini ya *EDF* kama zimetolewa chini ya *EDF* fulani kama 8, 9, 10, 11 kama fedha zile hazikutolewa zilikuwa zinasogezwa mbele bado ni zako zimekuwa *allocated* kwa nchi tuseme Tanzania.

Lakini baada ya hapo, baada ya kuanzisha kitu kinaitwa *Budget Session of the European Development Fund* mambo yamekuwa magumu zaidi. Wakikupa fedha na kwa sababu ya *capacity* ndogo hukuzitumia hizo fedha zinarudishwa kwenye mfuko mkuu kule *Brussels*. Hizo fedha zinaweza zinakuwa *allocated* tena zikatumika kwa utaratibu mwingine. Huu ni utaratibu mgumu sana kwa nchi nyingine zimepinga *Budget Session process* ya *EDF*. Kwa hiyo, sio kweli kwamba fedha zinakuja tu kirahisi kama tunavyofikiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha pili na ambacho ni muhimu sana ni utaratibu wa *negotiations*. Ninyi wenzangu mliponichagua mimi nilichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *Negotiations* zote za *Economic Partnership Agreement* kule *Brussels*. Hata baadhi ya Wabunge, wameniuliza wamesema wewe kwa nini unasafiri sana? Kwa nafasi yangu ya kuwa Mwenyekiti wa *Negotiations* wa *Economic Partnership Agreement* mimi nahudhuria Mikutano yote ya *Negotiations* zote za *Economic Partnership* za *Chief Negotiators* wa *configurations* zote ambazo ndugu yetu wa Upinzani alikuwa anaziita kanda. *(Makofi)*

Kuna Kanda ya *Pacific*, Kanda ya *Californium*, Kanda ya *ECOWAS*, Kanda ya *CEMAC* ambayo ni *Central Africa*, Kanda ya *ESA*, ambayo ni *Eastern and Southern Africa*, Kanda ya *SADC* zote hizi zinajumuishwa pamoja na *ACP Secretariat* na wale watu wenyewe wahusika wa *European Commission* katika majadiliano maalum ambayo yanaendelea. Katika majadiliano yote ambayo yanafanyika na *ASP Countries* wanakuja kwenye mazungumzo. Bahati mbaya sana mazungumzo yote yuko-*focused towards trade*.

Suala la *development dimension has not been addressed*. Yamekuja masuala ya kisiasa ambayo sasa yameingilia pale kwamba kama nchi ambazo zimeanzisha kanda hizi kwamba inaruhusiwa kuingia kwenye kanda moja tu na hii kanda moja ndiyo itawezesha kuwafanya wao waingie kwenye *free trade area (FTA)*. Masuala yenyewe kidogo ni *technical*. Lakini ni kwamba wewe huwezi kuwa *East African Community* ukasaini *agreement community*, ukasaini *agreement* ya *Free Trade Area*, ukaenda *SADC* watakapokuwa ni *Free Trade Area* ukasaini nyingine, ukaenda labda pengine tena ukasaini nyingine huwezi! Haiwezekani! Kama ilivyokuwa kwenye *COMESA*, labda upate bahati katika nchi ambazo zina *COMESA*. Nchi nyingi ambazo ziko kwenye *COMESA* ndizo ambazo zimeingia kwenye *ESA*. *Of course* pamoja na nchi nyingine ambazo zilikuwa *SADC* wote wamekwenda huku juu.

Sasa nayasema haya ili nije niseme hii ina maana gani kwa Tanzania? Tanzania sisi tumesaini mkataba na *East African Community* na tumeingia kwenye *Free Trade Area* kwenye *Customs Union*. Chini ya *SADC* tuna mpango mwingine ambao mwaka 2008 utatuingiza kwenye mpango kama huo. Sasa wale wanasema ahaa, lakini kwenye Mkataba walisema kazi ya hii *Agreement*, *The Cotonou Partnership Agreement will be to strengthen Regional Integration.* Lakini wewe unaniambia hapana huku usiweko na huku usiweko. *(Makofi)*

Sasa Tanzania sisi tunafaidika namna gani? Tanzania tumesaini kama nilivyosema *East African Community* na tunataka kwenda *SADC* au tume- *configure SADC*. Bahati mbaya sana *observer* aliyekuwa anashiriki na sisi alikuwa ni *South Africa* yeye sio *Member* wa *SADC*. Yeye ni *observer*, *South Africa has an independent Agreement with the European Commission* inayoitwa *The Trade and Development Corporation Agreement* ambayo ndiyo hiyo hiyo sawa sawa na hizi tunazozungumzia.

Lakini *South Africa* ana wenzake ambao wanazungukwa yaani wako *embedded* katika *Customs Union* ambaye inawaunganisha na wale wa kusini ambao tuko pamoja katika *SADC* ambao ni Botswana, Namibia, Lesotho, Swaziland na wale *Secretariet* yetu sasa iko Botswana. Sasa Botswana, Swaziland, Namibia na Lesotho wao wanasema ahaa, sisi hatuhitaji ku-*negotiate* na hii nyingine. Tutachunguza vipengele vya *TDCA* tuone vipi havitufai na vipi vinatufaa na tunaingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilipokuwa *Berlin* wamekuwa *very frantic, very clear* kwamba sasa sisi tunakwenda kuchambua mkataba wa *TDCA* ili tuungane na *South Africa*. Kwa hiyo, kwa maneno mengine *South Africa* itakuwa imechukua ile *configuration* ya *SADC*. Angola, Tanzania na *Mozambique* zinabaki hazina pa kwenda maana nchi nyingine kama Zimbabwe pamoja na Zambia na Malawi wameingia (*ESA) Eastern and Southern African Configuration*. Tanzania ndiyo tunasema tuko huko lakini kule hatuko. Sasa maoni yaliyoko ni kwamba, aidha tunaungana na wenzetu ambako tumesaini *Customs Union* ambao ni *ESA* ambao ni *Members* wa *COMESA*. Sasa sisi tunaona kigugumizi kwa sababu tulikwishajitoa *COMESA* tunaona kigugumizi sasa kusema tunarudi huko.

Hatua ya kwanza ambayo tunaweza kuchukua bado tunaweza ku-*negotiate under ESA* ambako kuna *benefits* zaidi kuliko tutakazozipata kwa Afrika Kusini. Mali Tuki-*form trade agreement* hii kupitia *South Africa,* sisi tutakuwa tumesaini *via the back door*. *Benefit* hazitakuwa (*directly)* moja kwa moja kuja Tanzania. Kwa sababu kwanza tuko mbali lakini pili Mali itakuwa inakwenda *South Africa Via the Agreement in South Africa*. Sijui kama nchi tatu zitaruhusiwa. *Alternative* iliyopo ni hizi nchi kuingia kitu kinaitwa *Everything But Arms (EBA).*

Lakini mnajua ninyi Waheshimiwa Wabunge na Serikali inajua kwamba, *we have always enjoyed* utaratibu wa *EBA* kwamba *special preferences have always been extended to Tanzania* chini ya utaratibu huo. Bado hatukufaidika kama ambavyo tungependa tufaidike katika utaratibu huo.

Lakini mwisho naomba niseme hivi, utaratibu wa ku-*negotiate* huu Mkataba umekuwa ni mgumu sana hivi sasa na nafikiri inavyokwenda *Barbados* kutatoka *statement* ambayo inaeleza *the difficulties* ambazo ni *embedded*. Nami *at some stage* nitawaandikia *report* ambayo inaonyesha baadhi ya mawazo ya *Council of Ministers* ambao ni *Chief Negotiators* wa kanda zao. Kila kanda ina Waziri ambaye ni *Chief Negotiator*. Kanda ya *SADC* Waziri wa Botswana ndiyo *Chief Negotiator* na kanda nyingine hizi zote zina Waziri ambaye anakuja ambao wiki iliyopita tulikuwa na Mkutano kule *Berlin*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule Mkutano umekuja na *special recommendations* ambazo zinaonyesha kwamba bado magumu, *European Commission must confirm* kwamba wanapenda ku-*negotiate* na sisi au hapana. Kama hawapendi *how do we proceed under the present circumstances?* Yako matatizo katika *negotiations* za Mkataba huu. Lakini *that is not with standing.* Bado Mkataba una manufaa na ni vizuri kuendelea ku-*negotiate* Mkataba huu. *That is the most important thing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayasema haya kwa sababu matatizo mawili yanayojitokeza makubwa sana ni kwamba tunapo-*negotiate* wao wana-*negotiate trade* zaidi *more than development*. Kwa hiyo, mipango yetu ya kuondoa umaskini bado inazuiliwa inakuwa *embed*. Sisi huu Mkataba tunautaka uondoe umaskini uliokithiri katika nchi zetu na yako matatizo mbalimbali ambayo tungependa kuyaondoa siyo yale tu ambayo ni *of interest to them.* Kwa haya ninayoyasema ndiyo baadhi ya matatizo ya *negotiations* katika Mkataba huu.

Kwanza, kwenye *level* ya *configurations,* lakini pili, kwenye *level* yenyewe tunapokwenda kusaini. Sasa hivi lugha inayozungumzwa kule ni lugha ya *Alternative Economic Partnership Agreement.* Sasa ukienda kwenye *Alternative,* nchi kama Tanzania pengine *capacity* yetu haitoshelezi na nchi nyingi za Kiafrika ku-*negotiate* hiyo *alternative will be quite difficult for us*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako matatizo mengi ambayo katika muda huu mfupi siwezi nikayaelezea, lakini ninahitaji muda zaidi ili niweze kueleza haya ili yaweze kueleweka vizuri zaidi. Yako matatizo makubwa katika *negotiations* katika Mkataba huu. Lakini Mawaziri wanajitahidi sana kuja na ufumbuzi ambao utasaidia nchi za *ACP*.

Naomba niseme, hivi Mawaziri wetu wanahudhuria Mikutano *at the level of the Council of Ministers?* Ninaomba sana wajenge tabia ya kuhudhuria Mikutano. Mikutano mingi ya *negotiations* hizi sisi hatuhudhurii *stake* yetu tunaiachia tu mikononi mwa wengine waamue sisi tutafuata, *it is not very good* na wenyewe wanajua. *(Makofi)*

Lakini pili, mpenda (*collaboration)* kushirikiana, mashirikiano kama Mtanzania anajua kitu tukae pamoja tujadili na tushirikiane kwenye *delegations* hizi. Kule *Brussels* wamesema, Wabunge washirikishwe sana katika mazungumzo haya kwa sababu *ultimately* wao ndiyo wanakaa kupitisha hii Mikataba. Lakini unapitisha Mkataba ambao hujui hatma yake kwa mwananchi, unamwakilisha ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo matatizo makubwa tunayoyapata. Sasa kama hamhudhurii, kama hamuendi ni kwamba *stake* ya nchi yetu *is left in the hands of other people* na mambo yanakwenda tu kama yanavyokwenda. Lakini tuhudhurie Mikutano yetu Watanzania. Sasa nafikiri *we have always been accepted* lakini wanaona kwamba hatuna *interest* kama tusipohudhuria vikao vikubwa au vikao vyenye manufaa makubwa kama hivyo. *(Makofi)*

Lakini mwisho, ninaomba Wizara ya Fedha iendelee kujenga *capacity* kwa watu wanaoshughulika na *EDF*. Ziko njia ambazo tunaweza kupata fedha zaidi chini ya mpango wa *EDF*. Hizo njia ni lazima watu wetu wawaruhusu wahudhurie vikao mbalimbali mahali popote vilipo, kwa sababu manufaa ni makubwa lakini hapa kwetu hujui anayehudhuria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Wizara ya Biashara pale anaweza kwenda mtu leo kesho sio yeye ni mwingine *different person or together* ukimwambia zungumzia masuala ya kumshauri Waziri hawezi, ni *very sub standard advice* anayopata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, ninaunga mkono Mkataba huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mporogomyi, Mwakilishi wetu kwenye Bunge la *ACP EU.*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita msemaji wetu wa mwisho, niwakumbushe Kamati ya Maliasili na Mazingira kwamba kutakuwepo Kikao kama kawaida saa saba kwa ajili ya kupitia hesabu za *Tanzania Wildlife Research Institute* za mwaka 2004/2005.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza ningependa ku-*declare interest,* kwa bahati nzuri kabisa Mheshimiwa Mporogomyi na mimi wote ni Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Mnaweza kuona jinsi Kamati ya Fedha na Uchumi inavyofaidika kwa kuwa na Mjumbe kama Mporogomyi. *(Makofi)*

Lakini kimoja kikubwa ambapo tulimwuliza Mheshimiwa Mporogomyi ni kwamba, taarifa zake zinaishia wapi? Akishatoka kwenye Kikao cha suala hili taarifa zake zinaishia wapi? Sisi tuliotia sahihi Mkataba na kuidhinisha Bungeni kusema sasa huo umeidhinishwa tunapataje taarifa hizo? Taarifa hizi Mheshimiwa Mporogomyi aruhusiwe yeye kuziandika kuzileta hapa. *Very interesting*, kwa sababu sasa hivi anapeleka Wizara ya Fedha na Wizara ya Fedha hawarudishi taarifa hizo kwetu. Sisi ndiyo tuliomchagua hapa kwenda kutuwakilisha. Kwa hiyo, mimi ningependa kwa mimi ningependa kwamba zile ambazo anapeleka Wizara ya Fedha vile vile nakala awasilishe Bungeni. Kwa sababu kwa taarifa kama hizi tutakuwa tunajua tunakwenda wapi, tunafanya nini. *(Makofi)*

Mkataba wa *Cotonou* ni Mkataba mzuri sana. Lakini kama hamfuatilii na kama mkiuacha tu nje uendelee, ninyi ni watu mnapigana vita ya uchumi bila ya kujua maadui zenu wana silaha gani. Tatizo moja kubwa sana bahati mbaya nitarudia mniwie radhi. Tatizo moja kubwa sana katika Mikataba hii kama nchi zenu haziendi kuhudhuria vikao, basi mtakuwa mnakandamizwa na mambo ambayo hata hayawahusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisome kipengele kimoja ambacho nchi zingeweza kufaidika na uniruhusu nisome kwa lugha ya Kiingereza, kutafsiri kwa Kiswahili hapa inawezekana nikababaisha tu. Kwenye Mkataba wenyewe ukurasa 54 (iii)

inasema: *“When an ACP states, State faces a crisis situation as the result of war or other conflict, or exceptional circumstances with a comparable effect preventing the National Authorizing Officer from carrying out his duty, the Commission may itself manage the resources allocated to the state in question in accordance with Article 3 and use it for special support”.*

Sasa hivi ni vitu ambavyo viko kwenye Mkataba huu, ni vitu ambavyo Wizara inatakiwa ivifuatilie. Ni vitu ambavyo nchi zinatakiwa zifaidike. Tunapokuwa na matatizo makubwa kwa mfano tulipata matatizo makubwa kabisa yaliyotokana na umeme na ukame tukawa na njaa, tukawa sasa umeme hatuna. Nilipowasiliana na watu wa *EU* wanasema kwa kipengele hicho kama nchi yenu ingeweza kuwasiliana na *EU* kwa hakika *negotiator* wenu angeweza kupata msaada unaotumika kwenye kipengele bure hicho ili *EU* kujaribu kuokoa hali halisi ya umeme nchini. Nadhani nikauliza wamekuja? Anasema nafikiri hawajakiona. *(Makofi)*

Sasa ni vizuri wenzetu wa Serikalini mtusaidie kweli kweli na sio vibaya basi mkaja mkatutengenezea semina za kutuelimisha kila wakati juu ya maazimio haya. Tunapitisha maazimio mengi na tukishalipitisha sisi hatujui linaendeleaje huko ili mradi tumesema hapa Bungeni ndiyo limepita. Lirudisheni kwetu kila wakati mtupe elimu. Msifikirie kwamba kila mkilipitisha hapa basi, sisi tunalifahamu. *(Makofi)*

Kwa bahati mbaya, nina miaka mingi na Wabunge wanaingia kila kipindi, wageni wengi sana ndani ya Bunge. Wenyeji wanakuwa wachache kwa hiyo, kuna haja ya kupatiwa elimu ya Mikataba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu unaweka mazingira ambayo sisi wenyewe tujisukume kuondoa umaskini. Mkataba huu una fedha za *STABEX*, uliweka fedha za kutengeneza barabara, uliweka fedha za kuendeleza kilimo cha kahawa, wale wanaolima kahawa. Lakini fedha hiyo, imechukua muda mrefu sana.

Nakumbuka katika kipindi cha miaka mitano tulikuwa tunazungumzia barabara za Mikoa, ambayo inalima kahawa. Tulikuwa tunazungumzia na kutupiana mpira ndani ya Serikali, mara Wizara ya Ujenzi ndiyo inayohusika, mara Kilimo ndiyo wanaohusika, mara Wizara ya Fedha ndiyo wanahusika. Ni vizuri tu tukaweka msimamo ni Serikali ndiyo inayohusika. Ni vizuri fedha hizi zikija zitumike. *(Makofi)*

Sasa wakati wote huo ndio sasa tunaanza kuzitumia fedha hizi wakati watu wamekata tamaa hata kulima. Kwa mfano, Milima ya Uluguru ilikuwa inalima kahawa, lakini kwa sababu ya kutokuwa na uhakika wa soko na bei kupungua watu wamefyeka mikahawa na kumbe kulikuwa na fedha za ku-*subsidize* kilimo cha kahawa. Lakini nani alijua, nani walielimisha, nani anafahamisha wakulima hawa kwamba mtafaidika katika misingi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ijaribu kutupa elimu kila wakati ili tuweze kujua ni nini cha kufanya hata Wabunge. Hasa Wabunge ndiyo wanatakiwa waelimishwe sana kwa sababu wao ndio wanaoulizwa maswali na *grassroots people*

kwenye *grassroots level* kule, wanaotakiwa kujibu ni Wabunge. Kwa hiyo, Serikali rudini kwetu mtuelimishe ili tujue sisi tukiuliza swali tunauliza kwa niaba ya wananchi waliotuchagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba huu una utaratibu ambao Mheshimiwa Mporogomyi aliusema. Zamani ulikuwa unaweza kupata fedha, kama hukuzitumia zinaendelea. Sasa ni mwaka hadi mwaka. Katika *EDF program* fedha zako utatumia kwa mwaka huo kwa *program* hiyo, kama hukuweza, fedha hizo ndiyo zimekwisha hapo. Sisi hatuwezi. Chukueni fedha, tumepewa kwenye *EDF* za kutengenezea barabara kutoka Dodoma kwenda Singida, barabara ni miaka mitatu inachukua, miaka miwili na nusu, miaka miwili. Sasa wenzetu wamekwenda kuweka *limit* kwamba fedha hizi unazopata lazima katika mwaka uzitumie wakijua fika kwamba uwezo wetu wa kiutalaam hautuwezeshi sisi kutengeneza barabara ama shughuli nyingine katika muda mfupi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikataba yetu ya kazi ina muda mrefu sana. Sasa matokeo yake sisi tunakwenda sasa kwenye unyonge kwa Mikataba, wanachokisema kwamba sasa lazima mrudi kwetu mtafute watalaam tuje tuwasaidie tena huko. Wanarudi kwa mlango wa nyuma. Tunapenda, hatupendi, misaada iko mingi, mikopo ipo mingi lakini kama hamwendi ku-*negotiate* kwamba mkopo huu katika *EDF* hii hatuwezi kutengeneza barabara kwa muda wa mwaka mmoja tunataka muda huo uongezwe na ninyi hamhudhirii, basi itabidi mfuate masharti yale ambayo kule *negotiator* amesaini.

Mimi ninawaomba tena ninawaomba sana wenzetu Wizara ya Fedha, ndiyo kinara wa kushughulikia Mkataba huu. Tulishalipitisha Azimio hili sasa tunarejea tu katika Azimio lile ambalo lilishapitisha. Ninawaomba sana waende na uwezo wa kutuwezesha Wabunge na kuwawezesha Watendaji Wakuu wapate elimu juu ya suala hili, wafuatilieje na wale ambao wanakwenda kwenye Mikutano ninaomba vile vile Wizara ya Fedha, wawe ni watu hao hao kufuatilia suala. Mchanganyiko wa mtu kwenda leo Juma, kesho kaenda John, keshokutwa kaenda Hamis inakuwa kufuatilia ni kazi sana. Kila mtu ana stahili yake kuandika ripoti.

Mimi nashukuru kwamba Bunge limekuwa na imani na Mheshimiwa Mporogomyi, kwa hiyo, anajua nini kinachoendelea kule, hebu kaeni naye chini basi mwambieni hebu njoo basi tukae chini sisi hapa tuna watalaam, tuambie mwenzetu matatizo gani angalau atuwakilishe sisi Wabunge huko kwenu, ndiyo tuliomchagua aende akatuwakilishe.

Lakini ripoti sisi hatupati mnazipata nyie, basi mkae naye chini halafu mtupe semina sisi na mpeni nafasi Mheshimiwa Mporogomyi, basi ile mnakuja kutupa semina/elimu na yeye awepo huko akiwa ni mtu ambaye anatuwakilisha atueleze ni nini. *(Makofi)*

Sasa hivi ametoa elimu hapa, amesema kwamba Wabunge wengi wako kwenye Mikutano saa hizi. Wachache wachache ndio tuko humu ndani. Kwa hiyo, itabidi waje kusoma kwenye *Hansard* na hiki ni kitu muhimu sana. Huu ni Mkataba muhimu sana kwetu. Naiomba sana Serikali ishughulikie. Mimi naujua sana huu Mkataba, niliusoma

wakati niko Wizara ya Ujenzi ndiyo unapata pesa nyingi sana za kutengenezea barabara na miradi mingine. Ziko pesa ili mradi mkiweza kuzungumza na ziko nchi tayari kusaidia, hata nje ya huo Mkataba ili mradi watu wakienda kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mengi ya kuongeza. Nilikwishasema tangu mwanzo kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati hii kwa hiyo nilikwishaujadili huu Mkataba kwa undani na nilitaka kuongezea tu na kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nawashukuruni sana Waheshimiwa Kilontsi Mporogomyi na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha. Sasa ni nafasi ya Mheshimiwa Waziri ku-*wind up* hoja yake ili tuweze kuendelea.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashukuru wale wote wamechangia katika hoja hii. Kwanza Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Fedha, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mwakilishi wa Kambi ya Upinzani - Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi ambaye ndiye Mwenyekiti mkubwa wa *negotiation* zetu ya hii *Cotonou Agreement* na mwisho Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi ya Fedha kwamba yale yote ambayo wametushauri wakati tuko kwenye Kamati yale ndiyo hasa bado aliyasisitiza na kwa hivyo hata ile hoja aliyotoa Mwakilishi wa Upinzani kwamba kuanzia mwaka 1975 mpaka hapa tulipofika kwamba tuna faida aina gani na hasara gani tunaipata, naahidi kwamba tunapata hasara zaidi lakini hatukupata lolote la maendeleo.

Lakini nasema kwa kweli tumepata kama alivyoainisha Mheshimiwa Hamza Mwenegoha kwamba kwa upande wa barabara kama mlivyoainisha, maana yake umaskini huchukui umaskini wa mfukoni tu, yaani wa fedha ya mfukoni. Unapoondoa umaskini ni kuwa na nyenzo ambayo zitakupelekea kuondoka katika umaskini, ambayo naamini kwa kiasi fulani kwa kiasi fulani imetusaidia sana hii *Cotonou Agreement* na namshukuru sana Mheshimiwa Mporogomyi, ameelezea kwa kirefu sana na kutokana na yale aliyoyaelezea na ushauri tulioupata kutoka kwenye Kamati, Serikali hasa Wizara ya Fedha imekubali kufanya Semina kuyaangalia haya kwa upana wake, faida za *Cotonou Agreement* na hasara zake ambazo zitaelezewa kwa urefu kabisa. Tutamwomba Mheshimiwa Mporogomyi awe ni mmojawapo wa watoa Mada wakati huo utakapofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaanza na Kamati ya Fedha na Uchumi na baadaye tutakuwa na Semina ya Bunge Zima kuhusu *Cotonou Agreement* kama ilivyo. Sio yeye tu, hata Mheshimiwa Zitto Kabwe ambaye pia ni Mbunge, amefanya kazi sana chini ya *EU Partnership Agreement* pia ni mmojawapo ambaye tutawaomba mshirikiane nasi katika Semina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi niseme kwamba ushauri tuliopewa na Waheshimiwa Wabunge tunaukubali na tutautekeleza na tutajitahidi kwamba wale wanaokwenda kwenye Mkutano huu wanakuwa ni watu wale wale, kwa Wizara ya Fedha siku zote mimi nimekwenda mara moja tu. Lakini zote Naibu wa upande wa pili ndiyo anahudhuria Mikutano yote wala haendi mtu mwingine.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti kwa ufupi nikuambie kwamba tunachukua ushauri wote tuliopewa na Waheshimiwa Wabunge na tutaufanyia kazi. Baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba kilicho mbele yetu ni hoja ya kuridhia marekebisho ya Mkataba wa Ushirikiano kati Jumuiya ya Ulaya na Nchi za Afrika, *Caribben* na *Pacific* au *Amendment of the Cotonou Partnership Agreement.*

Kwa hiyo, kwa hatua hii sasa kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alishatoa maelezo na akapitia zile kwa kuwa, kwa kuwa, madhumuni yote yale, suala lililo mbele yetu, sasa wajibu wangu mimi ni kuwahoji. Tukishamaliza hatua hiyo, tutakuwa tumeshamaliza hatua nzima ya upitishaji wa Azimio hili.

**Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Ushirikiano kati ya Jumuiya ya Ulaya (EU) na Nchi za Afrika, Pacific na Caribbean (ACP) (*Amendment of the Cotinuou Partnership Agreement)***

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio lililotajwa hapo juu liliridhiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mezani kwangu hapa sina tangazo lingine lolote. Palikuwa na watu wanaulizauliza kuhusu Semina ya tarehe 12 kama ni ya Kamati chache au Semina ya Bunge Zima. Nafikiri sote tulikuwepo na Mheshimiwa Spika alikwishaelezea kwamba ni Semina ya Wabunge wote. Kwa hatua hiyo tuliyofikia, basi naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 6.08 mchana Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu, Tarehe 12 Novemba, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*